- Sanctity**, n. utakatifu, usufi, utawa.
- Sanctuary**, n. mahali patakatifu, mahali pa ibada, moskiti, kanisa [*ma-*], hekalu [*ma-*]; (in a church) [*palipo mathbahu kanisani*]; (refuge) kimbilio [*ma-*].
- Sand**, n. mchanga; (fine) ufukwe; (sandy shore) ufuko.
- Sandal**, n. kiatu [*vi-*], kiatu cha ngozi.
- Sandal-wood**, n. sandali.
- Sandfly**, n. usubi.
- Sandglass**, n. [*chupa lenyi mchanga ndani, la kuonyesha saa ngapi*].
- Sandpaper**, n. [*karatasi yenye mchanga ya kulainisha mbau*], msasa.
- Sandpiper**, n. [*ndege ndogo ya pwanini*].
- Sandstone**, n. [*jiwe la mchanga uliogandamana*].
- Sandwich**, n. [*vipande vya mkate na nyama katikati*].
- Sandy**, a. -a mchanga, -enyi mchanga mwingi, -a rangi ya mchanga; (of soil) tifuufu.

- Sane**, a. *-enyi akili zake* [zao, &c.], *-enyi afya*.
- Saneness**, n. *kuwa Sane*.
- Sang**, p. t. *ya Sing*.
- Sanguinary**, a. *-kali, -a kufisha watu wengi, -a damu*.
- Sanguine**, a. *-tumaini, -a kutazamia mema tu, -a bidii*.
- Sanitary**, a. *-a kutia afya, -a mambo ya afya, kwa ajili ya afya*.
- Sanitation**, n. *kutia afya, maarifa ya mambo ya afya, kufanya mengi kwa ajili ya afya*.
- Sanity**, n. *kuwa na akili nzima, akili, busara*.
- Sank**, p. t. *ya Sink*.
- Sanskrit**, a. [lugha ya Wahindi wa kale].
- Sap**, n. *maji* [ya miti, majani, &c.], *utomvu*; (in war) *shimo* [handaki, ya kupenyzeza watu hatta boma la adui].
- v. *fukua mashimo* [handaki] *chini ya, ondoa misinji ya*; (weaken) *thoofisha, ondoa nguvu*.
- Sapience**, n. *busara, akili, ujuzi*.
- Sapient**, a. *-a Sapience*.
- Sapling**, n. *mti* [mi-] *mdogo, mti mchanga*.
- Saponaceous**, a. *-a sabuni, kama sabuni*; (flattering) *-a kujipendekesa*.
- Sapphire**, n. [johari ya thamani, sana, yenyi rangi ya samawati].
- Saracen**, n. *Mwislamu* [wa-] *wa kale*.
- Sarcasm**, n. [neni la kuchokozwa au la kuchoma moyo], *uchokozi, neno chungu, jibu kali, ubishi, matusi*.
- Sarcastic**, a. *-a Sarcasm, -kali*.
- Sarcophagus**, n. [jiwe la kuwekewa mayiti ndani, kama sanduku kubwa ya jiwe].
- Sardine**, n. [samaki ndogo tamu sana].
- Sardonic**, a. *Sardonic smile* (or laughter), [kucheka kwa uchungu, si kwa furaha].
- Sardonyx**, n. [kito kama Onyx].
- Sash**, n. *mshipi* [mi-], *mahazamu, masombo, ukumbuu*; (of win-
- dow) [dirisha la kuinuka na kushuka].
- Sat**, p. t. *na pf. t. ya Sit*.
- Satan**, n. *Shetani, Iblis*.
- Satanic**, a. *-a shetani, -a kishetani*.
- Satohel**, n. *mkoba* [mi-], *mfuko* [mi-], *bahasha*.
- Sate, Satiare**, v. *shibisha, kinaisha, vimbisha*.
- Satellite**, n. *mfuasi* [wa-] *mnyonge, mwandani* [wa-]; (star) [nyota mtoto].
- Satiation, Satiety**, n. *kushiba, kujivimbisha, shibe, ukinaifu, wingi*.
- Satin**, n. *italassi, kariri*.
- Satin-wood**, n. [mti laini wa kung'aa kama italassi].
- Satire**, n. (ridicule) *thihaka, mzaha, ubishi*; (invective) *ukali, masuto, matuso, maneno ya kushutumia kwa ukali*; (humour) *kuchekesha*.
- Satirical**, a. *-a Satire*.
- Satirize**, v. *fanyia Satire, thihaki, cheka, suta*.
- Satisfaction**, n. *kurithisha, kurithika*; (contentment) *urathi, raha mstarehe*; (payment) *malipo, malipizi*; (revenge) *kisasi*; (atonement) *kipatanisho*; (for murder) *dia*. It gave him great satisfaction, *ilimkalia tamu sana*.
- Satisfactory**, a. *-a kurithisha, -a kutosha, -a kuthubutisha, &c.*; (sound, trustworthy) *amini, -enyi sifa njema, -zuri*.
- Satisfied**, a. *rathi*; (with food) *-enyi kushiba*. Feel quite satisfied, *kinai*.
- Satisfy**, v. *rithisha, tuliza, tia urathi, ondolea mashaka, sterehisha, tosha*; (with food) *shibisha*; (with money) *lipa*.
- Satrap**, n. [liwali wa kiajemi wa kale].
- Saturate**, v. *nyweshwa maji mengi, lowesha kabisa, jaliza, nyweshwa sana*.
- Saturation**, n. [hali ya kunyweshwa maji mengi, &c. (Taz. Saturate)].
- Saturday**, n. *Juma a mosi*.
- Saturn**, n. [sayari moja] *zohali* (Ar.).
- Saturnalia**, n. [siku kuu kama siku

- ya mwaka, siku ya kufanya yo yote, kucheza, kulewa, jeuri, &c.*
- Saturnine**, a. -zito, -kali, -korofi.
- Satyr**, n. [zimwi la mwitu, jini].
- Sauce**, n. *mchuzi*; (impudence) *ujuvi, ubishi, ufithuli*.
- Saucepan**, n. (metal) *sufuria* [ndogo, *ya mkono*]; (earthen) *chungu* [vy-].
- Saucer**, n. *sahani ndogo, kisahani*.
- Saucily**, adv. *kwa ubishi, &c.* (*Tax. Saucy*).
- Sauciness**, n. *ubishi, ujuvi, &c.*
- Saucy**, a. -juvi, -bishi, -cheshi, -fithuli.
- Saunter**, v. *tembea, zunguka, enda polepole, tanga*.
- n. *matembezi, kujienda*.
- Sausage**, n. [maandasi ya nyama iliyokolewa, zaidi nguruwe].
- Savage**, a. -kali, -uaji, nduli; (rude) -shenzi; (desolate) *pasipo watu, ukiwa*.
- n. *mshenzi* [wa-].
- Savageness, Savagery**, n. *ukali, ushenzi*; (desolation) *ukiwa*.
- Savannah**, n. *poli* [ma-], *pululu* [ma-], *nyika* [ma-].
- Save**, v. *okoa, ponya*; (reform) *rudisha, tuliza*; (economize) *kabithi, weka akiba, weka*; (relieve) *achilia, punguzia kazi*. Save trouble, expense, &c., *punguza kazi* [gharama, &c.], *sayidia, faa*.
- Saving, Save**, prep. *illa, isipokuwa, japo, ghairi ya*.
- n. *kukata gharama, kujiwekea akiba, ukabithi*.
- a. -a *kuokoa, &c.* (*Tax. Save*).
- Savings**, n. *akiba ya mali, mapato*.
- Savings Bank**, n. [Bank ya kuwekea mali].
- Saviour**, n. *mwokosi* [wa-].
- Savour**, n. *luththa, utamu*.
- Savoury**, a. -tamu, -a *kunukia, -a kutamanisha, -liokolewa*.
- Saw**, n. *msumeno*; (maxim) *neni la fumbo, mithali*.
- v. *pasua kwa msumeno*.
- p. t. *ya See*.
- Sawdust**, n. [unga wa mbau, unga wa miti].
- Saw-fish**, n. [samaki mwenyi mdomo kama msumeno], *papa upanga*.
- Saw-mill**, n. [kinu cha kupasulia mbau, magogo, &c.].
- Sawn**, pf. t. *ya Saw*.
- Saw-pit**, n. [shimo la kupasulia mbau].
- Sawyer**, n. *mpasua mbau*.
- Saxon**, n. [Mwingereza wa kale].
- Say**, v. (p. t. *na* pf. t. *Said*) *sema, nena*. Say to, *ambia*. They say, It is said, *husema*. So to say, *kama vile*. Say, (perhaps) *huenda, labuda, kama*. That is to say, *maana yake, yaani*. I don't say, Not to say, *licha, sembuse*. Come along, I say, *njoo saa, twende wee*.
- Saying**, n. *neni* [ma-], *neni la fumbo, methali*.
- Scab**, n. *kigaga* [vi-].
- Scabbard**, n. *ala* [nyala], *uo* [nyuo].
- Scabby**, a. -enyi *Scab*.
- Scaffold, Scaffolding**, n. (building) *jukwaa* [ma-], *dungu* [ma-], *majengo*. Die on the scaffold, *kukatawa kitwa* [kusongwa, wazi mbele ya watu].
- Scald**, v. *unguza, choma, washa* [kwa maji ya moto]. Scalding hot, -a *moto sana*.
- Scale**, n. (measuring instrument) [kipande cha kupimia cheo ao kadiri]; (measure, degree) *cheo, kadiri*; (music) [jami ya sauti nane]; (of fish) *gamba* [ma-]; (of metal, mineral) *mavi*. Scales, *misani*; (dish) *kitanga* [vi-]. On a large scale, *kwa vikubwa*. On a small scale, *kwa vidogo*.
- v. *panda, kwea hatta juu ya*; (remove scales) *paa magamba*.
- Scalene**, a. (triangle) -enyi *pande zote tatu si sawa*.
- Scallop**, n. [kombe ya pwani].
- Scalp**, n. [ngoxi ya kitwani yenyi nyele, kishungi na ngozi yake], *utosi*.
- v. [kata shungi na ngozi yake].
- Scalpel**, n. *kisu* [cha kazi ya mganga].
- Scaly**, a. -enyi *magamba*.
- Scamper**, v. *enda mbio mbio, kimbia kwa tadi* [chap-chap], *puruka*.

Scan, v. *angalia, chungulia, tazamia*; (of verses) [*angalia mashairi kama yanakwenda vema na sawasawa, mashairi kwenda vema sawasawa*].

Scandal, n. [*nenobaya la kuchukiza*], *taksiri, neno la aibu, masingizio, maongezi mabaya, kikwazo*.

Scandalize, v. *chukiza, kosesha, kwaza*.

Scandalous, a. -a **Scandal**.

Scansores, a. [*ndege za kupanda miti kwa miguu*].

Scant, **Scanty**, a. -*chache, haba, kidogo*.

Scantiness, n. *uchache, ukosefu*.

Scapegoat, n. [*mbuzi mwenyi kuwekewa thambi za watu kiyahudi, kitu kilichotiwa hatiyani mahali pa ao badala ya watu wabaya, cha kusukumiziwa makosa*].

Scapegrace, n. -*baya, -potofu, -baa* [*ma-*].

Scapular, n. *kombe la mkono*.

Scar, n. *kovu* [*ma-*].

Scarce, a. *haba, -chache, shidda, ghali*.

Scarcely, adv. *shidda, si sana, kidogo*.

Scarceness, **Scarcity**, n. *shidda, uchache, njaa*.

Scare, v. *stusha, ogofya, tisha*; (drive away) *fukuza*.

— n. *hofu, fathaa*.

Scarecrow, n. *kitisho, kinyago*.

Scarf, n. (for waist) *deuli, mahazamu*; (for shoulders) *shali*.

Scarify, v. *chanja, piga mtai, papura, toja*.

Scarlet, n. [*rangi nyekundu kama bendera ao damu*], *wekundu*.

— a. -*ekundu*.

Scatheless, a. *pasipo hasara* [*mathara*].

Scatter, v. *tawanya, tapanya*; (sprinkle) *mwaga, nyrunyiza, rasha*; (disperse) *fukuza huko na huko*; (bring to nothing) *batilisha, haribu*. Be scattered (dotted about) here and there, *tapakaa*.

Scavenger, n. [*mtu mwenyi kufagia njia na kuondoa taka zote na kifusi*].

Scene, n. [*sehemu ya mchezo katika Theatre; matengeneo ya mchezo kama vinyago, mambo ya mchezo*]; (things seen) *mambo yenyeve, mambo yaliyooneka, vitu, hakika ya vitu*; (place) *mahali* [*palipofanyika mambo*]; (view) *suraya inchi*; (striking sight) *jambo la kutazamisha, tamasha*; (disturbance) *mambo ya ugomvi* [*hasira, huzuni*], [*mambo ya kutia kishindo ao fathaa*]. Be behind the scenes, *jua siri*.

Scenery, n. *tabia ya inchi, sura ya inchi*; (theatrical) [*matengeneo ya mchezo wa Theatre*].

Scenic, a. -a **Scene**.

Scent, n. *marashi, manuka, nukato* [*ma-*], *harufu*; (faculty of smell) *akili ya kunusa, nguvu ya kusikia harufu*; (track) *njia, nyayo, dalili*. Scent-bottle, *mrashi*. Be on the scent, *fuata nyayo* [*kwa kunusa*], *pata dalili*.

— v. *tia manukato katika, tia marashi*; (as a dog) *nukiza, nusa*.

Sceptic, n. *mtu wa Scepticism*.

Sceptical, a. -a **Sceptic**.

Sceptically, adv. *kama Sceptic*.

Scepticism, n. [*kushika na kuonya mashaka, kusema 'Sijui kama Muungu yuko, sijui kama mambo ya imani ni hakika'*], *mashaka*.

Sceptre, n. *fimbo ya mfalme, dalili ya enzi*; (sovereignty) *enzi*.

Schedule, n. *hati, daftari, hesabu, taarifu*.

Scheme, n. *shauri* [*ma-*], *kusudi, nia*.

— v. *fanya shauri, waza, kusudia*.

Schemer, n. *mtoa mashauri mengi, mtu wa hila*.

Scheming, a. -a *mashauri mengi, -erevu, -a hila*.

Schism, n. [*mtengano wa watu wenyi imani moja*].

Schismatic, a. -a *kushika Schism*.

Schist, n. [*jiwe gumu la kung'aa lenyi kupasuka upesi*].

Scholar, n. (learner) *mwana* [*wa-*] *chuoni, mwanafunzi*; (learned man) *mwalimu* [*wa-*], *mtaalamu* [*wa-*],

- mtu wa kulewa vema*; [*mtu mwenyi Scholarship* (endowment)].
- Scholarly**, a. -a *elimu*, -a *akili*, -*suri*, *halisi*.
- Scholarship**, n. (learning) *elimu*; (endowment of learner) [*malipizi ya mwana chuoni, fetha anayopewa apate kudumia mafundisho*].
- Scholastic**, a. -a *Scholar*, *Schoolmen*; (learned) -a *elimu nyingi*; (abstruse) -a *fumbo*, -*gumu kusi- kia*.
- Scholiast**, n. [*mwandikaji wa Scholium*].
- Scholium**, n. [*mafafanusi ya maneno ya vitabu vya kale*].
- School**, n. [*nyumba mnamosomesha watoto na kufundishwa*], *madrasa, chuoni, chuo*; (schoolboys) *jamii ya waanafunzi, waana chuoni*; (sect, opinions) *mathehebu, mafundisho*; (followers) *wafuasi*; (of fish) *kundi* [*ma-*], *wingi*. He has learnt in the school of experience, *amejua mambo ya ulimwengu*.
— v. *fundisha, ongoza, rudi*.
- Schoolman**, n. [*mwalimu wa kale, A. D. 1000-1500, katika Ulaya*].
- Schoolmaster**, n. [*mkuu wa School*], *mwalimu* [*wa-*].
- Schooner**, n. [*jahazi ya milingote miwili*].
- Sciatica**, n. [*ugonjwa wa mshipa wa upaja mbele ukiima*].
- Science**, n. (true knowledge) *elimu, maarifa, ujuzi wa hakika, elimu ya kweli*; (physics) *elimu ya ulimwengu na viumbe vyote; maarifa ya jamii ya vitu fullani*; (men of science) *watu wa elimu*. The science of Geology, *maarifa ya mawe*. Science tells us, *waalimu wa akili husema*.
- Scientific**, a. -a *Science*, -*juzi*.
- Scimitar**, n. *kitara* [*vi-*].
- Scintillate**, v. *metameta*.
- Scintillation**, n. *kumetameta, kime- tameta*.
- Sciolism**, n. *ujuvi, elimu kidogo*.
- Sciolist**, n. *mjuvi* [*wa-*].
- Scion**, n. *mtoto* [*wa-*], *mwana* [*wa-*].
- Scissors**, n. Pair of scissors, *makasi*.
- Scoff**, v. *thihaki, bishia, cheka*.
— n. *neno la thihaka* [*lakutharau*].
- Scoffer**, n. *mtu wa thihaka, mtu wa tharau*.
- Scold**, v. *karipia, kemea, shutumu*.
— n. [*mwanamke mkorofi mwenyi kukaripia, &c.*].
- Sconce**, n. [*kipande cha kukazia meshmaa ukutani, mwango*].
- Scoop**, n. (metal) *kombe, ukombo, bambo*; (ladle) *kata* [*ma-*], *upawa* [*pawa*]; (spoon) *mwiko* [*mi-*].
— v. (hollow out) *komba*; (by digging) *fukua*; (of water) *kumba*.
- Scope**, n. (range, room) *eneo, upeo, nafasi, mahali*; (power) *nguvu, akili*; (purpose) *shauri, kusudi*.
- Scorbutic**, a. -a *Scurvy*.
- Scorch**, v. *unguza, choma, umiza* [*haribu*] *kwa moto*.
- Score**, n. (account) *hesabu*; (twenty) *asharini, korja*; (line) *mfuo* [*mi-*]; [*andiko la, harufu za, Music*]. On the score of, *kwa sababu ya*.
- Scores**, *wingi*.
— v. *pata hesabu, pata fayida*; (cut into) *kata, chora*. Score off, *shinda, fayidia*.
- Scorer**, n. *mwandikaji wa hesabu* [*za mchezoni*].
- Scoria**, n. *mavi ya chuma, takataka za madini, mawe yaliyoyeyuka*.
- Scorn**, n. *tharau, thihaka, kiburi*.
— v. *tharau, tweza, cheka*.
- Scorner**, n. *mwenyi kutharau, mtu wa kiburi*.
- Scornful**, a. -a *kutharau*. Scornful abuse, *matwasi*.
- Scorpion**, n. 'nge.
- Scot, Scotchman**, n. [*mtu wa Scotland*].
- Scot-free**, a. *pasipo hasara, salamu salimini, pasipo kulipa*.
- Scoundrel**, n. *mtu mbaya kabisa, ragai, baa*.
- Scour**, v. *sugua sana, safisha kwa kusugua, parusa*; (pass quickly over) *pitia mbio*.
- Scourge**, n. *mjeledi* [*mi-*] *wa ngozi*; (punishment) *athabu, malipo, ki-*

- sasi*; (plague) *pigo* [ma-], *msiba mkuu* [mi-].
- Scourge**, v. *piga*, *rudi*, *patiliza*, *athibisha*.
- Scout**, n. *mpelelezi* [wa-], *mdukizi* [wa-]; (servant) *mtumishi* [wa-].
— v. *peleleza inchi*; (disdain, reject) *cheka*, *tharau*, *kataa kabisa*.
- Scowl**, v. *kunja uso*, *tazama vikali*.
— n. *uso wa kukunjamana*, *uso mkali*.
- Scrag**, n. [*kipande kibaya*].
- Scraggy**, a. *-baya*, *-embamba*, *-a kukonda*, *-gofu*, *-chache*.
- Scramble**, v. *enda kwa miguu na mikono*, *enda kwa shidda*, *tambaa*; (struggle) *songana*, *shindana*.
— n. *uchafuko*, *fujo*, *mwendo wa shidda*, *mashindano*.
- Scrap**, n. *kipande kidogo*; (of food) *kombo* [ma-].
- Scrape**, v. *para*, *paruza*; (outside) *puna*, (of fish, vegetables) *paa*; (inside) *kwangua*, *komba*, (of coconut) *kuna*. Scrape along, *kwaruza*, *enda kwa shidda*. Scrape past, *ambaa*. Scrape together, *kusanya kwa shidda*, *pata kwa nguvu*. Scrape acquaintance, *jipendekeza*.
— n. *uparuzo*, &c. (*Tax. Scrape*, v.); (difficulty) *shidda*, *mashaka*, *hatari*, *msiba* [mi-]. Be in a scrape, *kwama*.
- Scraper**, n. [*mtu wa, kitu cha, kuparuza*, &c. (*Tax. Scrape*, v.)], *kisu*, *ukombo*, *mbuzi*, &c.
- Scrapings**, n. *matakato*, *makombo*, *vidogo*, *takataka*.
- Scrappy**, a. *vivi hivi*, *ovyo*, *-siotengenaea*.
- Scratch**, n. *mtai* [mi-], *choro* [ma-], *mfuo* [mi-]; (in games) *mstari* [*pa kuanzia*], *mwanzo*; (tattoo) *tojo*. Come to the scratch, *jiweka tayari*, *shika kazi*, *kaza shauri*.
— a. *-a bahati*, *-a watu wo wote*, *ovyo*.
— v. *kuna*, *kunyua*, *piga mtai*, *papura*, *pelekea makucha*; (tattoo) *toja*, *chanja*; (with tool, pen, &c.) *chora*; (in racing) *toa katika mchezo*; (like a horse, fowl, &c.) *para*. Scratch out, *futa*. Scratch a hole, *fukua*.
- Scrawl**, v. *andika vibaya*, *chora*.
— n. *mwandiko mbaya*, *mchoro*.
- Scream**, n. *kilio cha nguvu*; (for help) *kiowe* [vi-]; (for joy) *kigelegele* [vi-].
— v. *piga Scream*, *lia*.
- Screech**, n. *na v. kama Scream*.
- Screech-owl**, n. *bundi*.
- Screen**, n. *kisetiri*, *kifuniko*, *kificho*, *ukingo*; (wall) *kiwambaza*; (shield) *ngao*, *kigao*; (hanging) *pazia*; (something stretched tight) *kiwambo*; (concealment) *kificho*, *maficho*; (forsifting) [*kama kayamba kubwa*].
— v. *setiri*, *funika*, *ficha*; (protect) *linda*, *okoa*, *tunza*, *hifathi*.
- Screw**, n. *parafujo*; (of ship) [*Tax. Screw-propeller*], *pepeo*, *cherehe*, *mapanga*; (miser) *bakhili*, *ntosa fetha nyingi*, *mgumu*. A screw loose, *kipunguo*, *kosa*; (mental) *kichaa*. Put the screw on, *lazimisha*, *kaza*.
— v. *tia Screw*, *kaza kwa Screw*; (squeeze) *songa*; (extort) *toza* [*fetha ao kazi kwa nguvu*], *lazimisha*. Screw up courage, *piga moyo konde*, *kaza moyo*.
- Screw-driver**, n. [*kipande cha sere-mala cha kuzungushia parafujo*].
- Screw-propeller**, n. [*gurudumu la nyuma la kuendesha merikebu ya moshi*], *cherehe*, *pepeo*, *mapanga*.
- Screw-steamer**, n. [*merikebu ya moshi yenyi Screw-propeller*], *meli*.
- Scribble**, v. *andika upesi*, *andika vibaya*, *chora*.
— n. *mwandiko wa haraka*, *mwandiko mbaya*, *mchoro*.
- Scribbler**, n. *mwandika ovyo*, *mwandishi hafifu*, *mchorachora*.
- Scribe**, n. *mwandishi* [wa-], *karani* [ma-], *katibu*.
- Scrimmages**, n. *mapigano*, *machafuko*.
- Scrip**, n. *hati*, *cheti*; (wallet) *kifuko*, *mkoba*.
- Scriptural**, a. *-a Scripture*, [*-enyi kupatana na maneno ya Scripture*].

Scripture, n. [*maandiko matakatifu, jamii ya vitabu vya kanuni vya kimasihya, maneno ya Bible*].

Scrivener, n. *mwandishi* [wa-], *karani* [ma-], *katibu*.

Scrofula, n. [*ugonjwa wa kuvimba shingoni na vifungoni*], *halula, marathi ya mti*.

Scrofulous, a. *-enyi Scrofula, -a Scrofula*.

Scroll, n. [*hati ya kukunjika, hati ndefu*].

Scrub, n. *msitu, koko, makoko, magugu*.
— v. *sugua sana*.

Scrubby, a. *-enyi Scrub*; (slight, paltry) *-nyonge, hafifu, -dogo, -baya*.

Scruple, n. *shaka* [ma-], *waswas, shidda*; (measure) [*kipimo kidogo cha uzito chenye 20 Grains*].
— v. *si kubali, si penda, si rithia*.
He scruples to go, *hataki kwenda, aenda kwa shidda*.

Scrupulous, a. *-a kutaka hakika, -a kufanya barabara, -a hathari, halisi*; (exacting) *-enyi mifundo* [*kusita, hofu*], *-bishi, chaguzi*.

Scrupulousness, Scrupulosity, n. *kuwa Scrupulous, uangalifu*.

Scrutinize, v. *chungulia, angalia sana, tazamia*.

Scrutiny, n. *kuchungulia, &c.*

Soud, n. *ukungu, umande, kiwingu*.
— v. *chukuliwa upesi na pepo*.

Scuffle, n. *ugomvi, mapigano, mashindano*.
— v. *shindana, pigana*.

Scull, n. *kasia* [ma-] *dogo*.
— v. *piga kasia*.

Sculler, n. *mpiga kasia*.

Scullery, n. [*pa kuoshea sahani na vyombo vya kupikia*].

Sculptor, n. *fundi wa kuchora* [wa *nakshi*].

Sculpture, n. *mchoro, kazi ya kuchora, nakshi, sanamu ya mchoro*.

Scum, n. *povu, fuo, takataka za juu* [ya *maji, &c.*] *kufu, koga, gaga*.

Souper, n. [*kitundu mbavuni mwa merikebu na sitahani cha kuchuruzikia maji*], *kipenyo*.

Sourf, n. *vigaga*.

Scurrility, n. *matukano, matusi*.

Scurrilous, n. *-a kutukana, -a matusi*.

Scurvily, adv. *vibaya*.

Scurvy, n. [*ugonjwa kama Scrofula*].

— a. *-nyonge, -baya*.

Scuttle, n. [*tundu mbavuni mwa merikebu ao sitahani la kupenya watu*]; (for coals) *kopo* [*ndoo, ya kuweka makaa*].

— v. *kimbia, fanya haraka*; (cause to sink) [*samisha chombo kwa kutoboa chini*].

Scythe, n. *mundu* [mi-, *mkubwa wa kukatia majani*].

Sea, n. *bahari*; (wave) *wimbi* [ma-]; (abundance) *wingi*; (disturbances) *machafuko*. At sea, *baharini*; (perplexed) *-enyi mashaka*. Heavy sea, *mawimbi makubwa*. Go to sea, *-wa baharia*.

Sea-anemone, n. [*mnyama kama ua likiota baharini*].

Sea-board, Sea-coast, n. *inchi kari-bu ya bahari, upande wa pwani*.

Sea-faring, a. *-enyi kazi chomboni, -a kukaa baharini, -a bahari*.

Sea-faring men, waanamaji, mabaharia.

Sea-girt, a. *-liozungukwa na bahari*.

Sea-green, a. *-a rangi ya bahari*.

Sea-horse, n. = **Walrus**.

Sea-kale, n. [*mboga ya pwani*].

Sea-king, n. [*haramia wa Norway zamani*].

Seal, n. *muhuri* [*muhuri, mihuri, chapa, alama*]; (sanction) *usakihi, ithini, ruksa*; (animal) [*nyama wa bahari yenye ngozi ya manyoya mazuri sana*].

— v. *tia muhuri, &c.* Seal up, *ziba, funga*.

Sealer, n. [*mtu, ao chombo, wa kuwindia Seal*].

Sea-level, n. [*sawa na juu ya bahari*].

Sealing, n. *kuwinda Seal* [*nyama*].

Sealing-wax, n. *lakiri*.

Sea-lion, n. [*nyama wa bahari kama Seal*].

Seam, n. *mshono* [mi-]; (tacked) *bandi*; (strong) *jongo*; (hemmed)

upindo; (of coal, metal) [*makaa, madini katika mwamba*]; (in ships) *kiungo, ufa* [*kati ya mbau*].
Seaman, n. *baharia, mwana maji* [*wa-*].
Seamanship, n. *maarifa ya kazi ya jahazi*.
Seamstress, n. *mshoni* [*mwanamke*].
Seamy, a. *-baya, -kukuu*.
Sear, v. *choma, unguza, kausha, fanya -kavu*.
Search, v. *tafuta katika, pekua, pe-leleza, sapa*. Search for, *tafuta, tazamia*.
 — n. *kutafuta, upelelezi, &c.*
Searcher, n. *mwenyi kutafuta, mpelelezi, mpekuzi*.
Searching, a. *-a kujaribia zote, -a kupenya ndani, -kali*.
Search-light, n. [*taa kubwa ya kung'aza usiku*].
Search-warrant, n. *ruksa ya serkali* [*kutafuta ndani ya nyumba*].
Sea-room, n. [*kuwa mbali na pwani*].
Sea-serpent, n. *joka kubwa la bahari*.
Seashore, n. *ukingo wa bahari, ufuko*. On the seashore, *pwani*.
Seasick, a. *-enyi Sea-sickness*.
Sea-sickness, n. *ugonjwa* [*taabu*] *ya bahari, kuchafuka tumbo* [*kutapika*] *chomboni, kulewa bahari*.
Seaside, n. *upande wa pwani, ukingo wa bahari*. At the seaside, *pwani*.
Season, n. *wakati, wakati wa mwaka, majira, muhulla*. The seasons, *pembe za mwaka*. It is in season, *ni wakati wake, yapatikana*. The wet season, *masika, siku za mvua*. The cold season, *kipupwe*.
 — v. (food) *kolea, unga, tia kitoweo, tia kiungo*; (fit for use) *tengeneza, tia dawa*; (accustom) *zoeza*.
Seasonable, a. *-a kufaa, kwa wakati wake, sawasawa*.
Seasoning, n. *kukolea, &c.* (*Taz. Season, v.*), *kitoweo, kiungo*.
Seat, n. (chair, stool, &c.) *kiti* [*vi-*]; (of earth, stone, &c.) *baraza, kibaraza*; (stone bench) *ufunga*; (but-tocks) *matako*; (on horseback)

kupanda frasi; (residence) *nyumba, mahali, pa kukalia, kikao, makazi*. Take a seat, *keti, kaa kitako*.

Seat, v. *ketisha, kalisha, weka, -pa kiti, wekea viti*. Seat oneself, *kaa kitako, keti, starehe*. I am seated, *nimekaa*.

Seaward, a. *-a upande wa bahari*.

Seaweed, n. *mwani, maua ya pwani*.

Seaworthiness, n. *kuwa Seaworthy*.

Seaworthy, a. (of ship) *-zima, -ema, -a kwenda baharini*.

Secede, v. *jitenga, jitoa, farakana, ondoka*.

Seceder, n. *mwenyi kujitenga, &c.*

Secession, n. *kujitenga*.

Seclude, v. *tenga, funga, farakisha*.

Secluded, a. *-a faragha, -a mbali, pasipo watu, -a uta'wa*.

Seclusion, n. *faragha, kujitenga, maficho, upweke, uta'wa*. Live in seclusion (indoors), *ta'wa, jitenga*.

Second, a. *-a pili, -a baadaye, -a mbele, -a chini*. On second thoughts, *baadaye, kisha kufikiri*. It is second to none, *haipitikani kabisa, hakuna bora zaidi*.

— n. (supporter) *rafiki, msayidia*; (moment) *dakika, nussu dakika*. [*sehemu ya settiniya Minute moja*] In a second, *ghafala, marra moja*. Second hand, [*mkonono wa saa wenye kuonyesha Second*].

— v. *sayidia, tia moyo, sema mama moja na, taka mama moja na*.

Secondary, a. *-dogo, hafifu, -baya, si bora*; (succeeding) *-a kufuata, -a namna ya pili, -a baadaye*.

Seconder, n. *mwenyi kusayidia* (*Taz. Second, v.*).

Second-hand, a. *si -pya, -liokwisha tumika, -a kuuzwa marra ya pili*.

Secondly, adv. *ya pili, tena, baadaye*.

Second-sight, n. *utabiri, akili ya kujua yatakayokuja, uaguzi*.

Secrecy, n. *siri, faragha, maficho, kusetiri*.

Secret, n. *siri, jambo la siri, fumbo*. In secret, *kwa siri, faraghani*.

- Secret**, a. -a siri, -a faragha; (faithful) -a kushika siri, amini.
- Secretary**, n. katibu, karani, mwandishi [wa-]. Secretary of State, waziri [ma-].
- Secrete**, v. fanya [fanyiza] **Secretion**; (hide) ficha, setiri.
- Secretion**, n. [kitu cho chote (maji, damu, mate, shahamu, belghamu, yo yote) kilichofanyizwa ndani ya mwili wa mwenyi uzima, nyama, mdudu, mmea, &c.; kufanya au kufanyiza ndani ya mwili]; (hiding) kuficha, kusetiri.
- Secretly**, adv. kwa siri.
- Secretory**, a. -a kufanya **Secretion**.
- Sect**, n. matkehebu, mathhabu, watu wenyi shauri moja; (religious) [jamii ya watu waliotengana na Kanisa la kimasikiya].
- Sectarian**, a. -a Sect.
- Sectarianism**, n. [kufuatana na Sect, kupendana na Sect].
- Sectary**, n. [mtu wa Sect].
- Section**, n. mkato [mi-], sehemu, fungu [ma-], nussu; (of soldiers) kikosi [cha asikari]; (of book) jusuu, fungu [ma-], gombo [ma-].
- Sectional**, a. -a Section.
- Sector**, n. (of circle) [sehemu ya duara kati ya Radius mbili].
- Secular**, a. (worldly) -a ulimwengu huu [sio -a dini]; (lay) -a watu tu [sio -a padre]; (profane) kama walimwengu, -a matumizi ya siku zote; (periodical) -a miaka mingi, -a wakati wake.
- Secularism**, n. [tabia na desturi zilizo Secular, tabia ya ulimwengu].
- Secularity**, n. [hali ya kuwa Secular].
- Secularize**, v. fanya Secular, tenga na mambo ya dini, twalia Kanisa [mali, &c.].
- Securable**, a. (to be made safe) -a kufanyika salama; (to be made fast) -a kukazika; (to be got) -a kupatikana.
- Secure**, a. (safe) salamu, pasipo hofu, pasipo mashaka; (reliable) amini, -aminifu; (certain, sure) -a hakika, yakini, thabiti.
- Secure**, v. weka salamu, tunza, linda; (fasten) funga, kaza; (get) pata, jipatia, miliki.
- Security**, n. salama, raha, kustarehe; (feeling safe) kuwa pasipo hofu [mashaka]; (guarantee) amana, rahani; (personal) mthamini [wa-]; (bond) kati, sharti.
- Sedan-chair**, n. [kama machela].
- Sedate**, a. -tulivu, -pole.
- Sedative**, a. -a kutuliza.
- Sedentary**, a. -a kukaa kitako, -a kukaakaa.
- Sedge**, n. manyasi [majani] ya mtoni.
- Sedgy**, a. -enyi Sedge nyingi.
- Sediment**, n. mashapo, takataka za chini, matope ya mto, tamma.
- Sedimentary**, a. -a Sediment.
- Sedition**, n. fitina, maasi.
- Seditious**, a. -a Sedition.
- Seduce**, v. longoza; (corrupt) poteza, vuta kwa mabaya, kossha.
- Seducer**, n. mdanganya, mpotezi; (of women) mtongozi.
- Seduction**, n. kupoteza, ushaushi; utongozi.
- Seductive**, a. -a kudanganya, -a kuvuta. -a kupoteza.
- Sedulity**, n. kuwa Sedulous, bidii.
- Sedulous**, a. -tendaji wa kazi, -a kushika kazi, -angalifu, -a bidii.
- See**, v. (p. t. Saw, pf. t. Seen) ona, tazama; (understand) fahamu, tambua, elewa; (experience) -wamo; (visit) amkia, enda tazama; (accompany) shindikiza, peleka. See off, shindikiza. See to, See about, See after, angalia, tengeneza. See through, See out, angalia, linda hatta mwisho, elewa -ote. See (a person) off (on a journey, &c.), safirisha; (after a visit) shindikiza. Seeing that, kwa kuwa, kwa maana, ikiwa.
- n. = Diocese.
- Seed**, n. mbegu, mbeyu; (origin) asili, mwanzo; (offspring) msao, mtoto [wa-]. Run to seed, haribika, chakaa.
- v. toa mbegu.
- Seedling**, n. mche [mi-].

Seedsman, n. *mwuza mbegu*.
Seed-time, n. *majira ya kupanda*.
Seedy, n. *-gonjwa, -kukuu, -a kuchakaa*.
Seeing, n. *kuona kwa macho, nguvu ya kuona*.
Seek, v. (p. t. na pf. t. Sought) *tafuta, tazamia, omba*.
Seem, v. *onekana, -wa na mfano wa, -wa kama, fanana na*. It seems so, *naona, labuda, huenda*.
Seeming, a. *-a uwongo, -a kujifanya, si kweli, si halisi*.
Seemingly, adv. *kama, kwa sura, kwa kuonekana, kwa nje*.
Seemliness, n. *kuwa Seemly*.
Seemly, a. *-suri, -a adabu, -a kustabili, -a kufaa, wajibu*.
Seen, pf. t. *ya See*.
Seer, n. *mnajimu [wa-], mwaguzi [wa-], mwenyi kutabiri, nabii*.
See-saw, n. [*kwenda na kurudi marra nyingi*; (game) *michezo wa watoto, kama pembea*].
Seethe, v. *tokosa, chemsha*; (neut.) *chemka, toa povu*.
Segment, n. [*sehemu ya duara, iki katwa na mstari*].
Segregate, v. *tenga, weka mbali, farikisha*.
Segregation, n. *kutenga, &c.*
Seize, v. (grasp) *kamata, shika, twaa, shikilia*; (take by force) *twa kwa nguvu, nyang'anya, pokonya*; (comprehend) *fahamu, elewa*.
Seizure, n. *kukamata, kukamatwa, &c.*; (attack of illness) *kushikwa na ugonjwa, kipindi*.
Seldom, adv. *shida, marra chache*.
Select, v. *teua, chagua*.
 — a. *-a kuchagua, -teule, haba*.
Selection, n. *kuchagua, &c.*; (portion) *nussu, sehemu [ya vitu vingi]*; (choice bits) *madondoo, mateuzi*.
Self, n. (pl. Selves) *moyo, nafsi, mwenyewe*; (in verbs) *-ji-*. He killed himself, *alijiua*. It goes by itself, *inajienda*.
Self-abnegation, n. *Taz. Self-denial*.
Self-acting, Self-adjusting, a. [-a

kutenda kazi peke yake], *-a kujienda*.
Self-assertion, Self-assurance, Self-complacency, Self-conceit, n. *ukinaifu, ukavu, kujiona*.
Self-confidence, n. *Taz. Self-reliance*.
Self-conscious, a. *-a kujifahamu nafsi, -a kujikumbuka, -enyi akili ya kujijua [hali, tabia, nafsi] na kujiongoza*; (shy) *-enyi haya*.
Self-consciousness, n. *kuwa Self-conscious*; (shyness) *haya*.
Self-contained, a. (independent) *-kinaifu*; (reserved) *-nyamavu*; (complete) *-a kujitosha, kamili, -enyi yote ndani yake, -a kujitoshela*.
Self-controlled, a. *-taratibu, -vumilifu, -tuliva*.
Self-conviction, n. *kujionya kuwa na kosa, kujifunga, kujihukumu*.
Self-dedication, n. *kujitoa, kujiweka -enyewe*.
Self-defence, n. *kujilinda nafsi, kujipigania*.
Self-denial, n. *kujihinisha, kujinyima, kujiweza, kujikania, kujizuia*; (temperance) *kiasi*.
Self-denying, a. *-a Self-denial*.
Self-destruction, n. *kujifisha, kujipoteza*.
Self-determining, a. *-onyi ihtiari, -enyi nguvu [akili] ya kuchagua*.
Self-devotion, n. *kujitoa, kujifunga kwa kazi*.
Self-educated, a. *-a kujifunza -enyewe tu, -liojelemisha pasipo mwalimu, -a kujihitimisha*.
Self-esteem, n. *kiburi, kujisifu, kujiona -ema*.
Self-evident, a. *waziwazi, baini, thahiri*.
Self-examination, n. *kujitazamia moyo, kujihoji nafsi, kujitafutia makosa ndani, kujishtaki rohani*.
Self-existence, n. [*hali ya kuwa Self-existent*].
Self-existent, a. (of God) *-sio na mwanzo wala mwisho, -enyi kuwa*

- yuko peke yake halisi, -a hakika; (uncreated) -sioumbwa. si kiumbe.*
- Self-government**, n. *kujiwexa nafsi, kujitawala -enyewe.*
- Self-importance**, n. *kama Self-assertion.*
- Self-indulgence**, n. *anasa, upotofu.*
- Self-interest**, n. *kujipatia fayida, kujipendexa nafsi, choyo.*
- Selfish**, a. *-a choyo, -a kujiangalia nafsi wala si mwenziwe, -a kujipendexa, -a kujipendelea nafsi, -a kushika lake; (grasping) -pasi; (miserly) bakhili.*
- Selfishness**, n. *choyo, kuwa Selfish.*
- Self-love**, n. *kujipenda nafsi; [kama Selfishness].*
- Self-made**, a. *-pasi, -liojipatia utajiri. A self-made man, masikini aliyejipasha utajiri.*
- Self-possessed**, a. *-a kujiwexa nafsi, -a kiasi, -kavu wa macho, -taratibu.*
- Self-possession**, n. *kuwa Self-possessed, macho makavu.*
- Self-reliance**, n. *kujijetea nafsi, kutotaka msaada, ukinaifu, ujasiri.*
- Self-respect**, n. *kujiheshimu nafsi [kadiri ipaswavyo, pasipo kiburi], kuchunga cheo.*
- Selfsame**, a. *-moja halisi, sawa sawa, yule yule [ile ile, &c.].*
- Self-satisfaction**, n. *kujiona, majisifu, ukinaifu.*
- Self-sown**, a. (tree) *kimelea [vi-].*
- Self-sufficiency**, n. *kinaya. ukinaifu; (pride) majivuno, kiburi.*
- Self-sufficient**, a. *-enyi Self-sufficiency.*
- Self-will**, n. *ukaidi, &c.*
- Self-willed**, a. *-kaidi, -shupafu, -asi, -potofu.*
- Sell**, v. (p. t. na pf. t. Sold) *uza, toa kwa fetha; (neut.) uzanya, usika; (deceive) danganya. Sell up, filisisha. Sell out, uza mali yote. Sell to, liza.*
- Seltzer**, n. [*maji ya Ulaya, maji ya pofupofu*].
- Selvedge**, n. *upinda.*
- Selves**, pl. *ya Self.*
- Semaphore**, n. [*mti wenyi vipande, kama mikono, vya kuashiria*].
- Semblance**, n. *mfano, sura, umbo.*
- Semen**, n. *shahawa.*
- Semi-**, *nussu, kidogo.*
- Semibreve**, n. *nussu Breve.*
- Semicircle**, n. *nussu halisi ya duara.*
- Semicircular**, a. *kama Semicircle.*
- Seminal**, a. *-a mbegu; (original) -a asili, -a mwanzo.*
- Seminary**, n. = **School**, *madrasa, chuo, chuoni.*
- Semsem**, n. *ufuta; (oil) mafuta ya uta.*
- Senate**, n. [*baraza kuu ya wazee*].
- Senator**, n. *mtu wa Senate.*
- Senatorial**, a. *-a Senator.*
- Send**, v. (p. t. na pf. t. Sent) *peleka, tuma, agiza; (cause to go) toa, tupa, rusha, endesha, sukuma, jongeza; (grant) jalia; (despatch messenger) tuma mtu. Send for, ita, tuma mtu kuita. He was sent for, alikwenda kwitwa.*
- Sender**, n. *mwenyi kupeleka, &c.*
- Seneschal**, n. *msimamizi wa nyumba [zamani za kale].*
- Senile**, a. *-a mzee, -a kizee.*
- Senility**, n. *uzee, ukongwe.*
- Senior**, a. *na n. -kubwa [kwa daraja, cheo, umri, &c.], -a kwanza.*
- Seniority**, n. *kuwa Senior; (rank) kadiri ya cheo, cheo.*
- Senna**, n. *sanamaki.*
- Sensation**, n. (perception by sense) *kuona; (excited feeling) kushtuka, kushtusha, fathaa, kishindo; (exciting object) kitisho, kituko, ajabu.*
- Sensational**, a. *-a kustusha, -a kutisha, -a ajabu.*
- Sensationalism**, n. [*kusema, 'Hatupati kujua neno illa kwa kiwiliwili; asili ya maarifa yote ni nje si ndani, ni katika vitu vyenyewe, si katika moyo na akili ya mtu'*].
- Sense**, n. *akili, busara; (meaning) maana; (perception) kuona [kwa macho, masikio, pua, ulimi, kugusa]; (opinion) shauri; (lower nature) mwili. Have a sense of, ona. The sense of smell, hearing,*

taste, &c., *kusikia, kuonja, &c.*
 A man of good sense, *mtu wa akili, hodari*. Pleasures of sense, *anasa za mwili*. In the sense of, *kwa maana, maana yake*. In the same sense, *kwa maana ile ile, maana sawa*. It has a bad sense, *maana yake mbaya*. The senses (five senses), *kuona kwa macho, kusikia, kunusa, kuonja, kugusa*; [*milango ya maarifa*]. Be out of one's senses, *Lose the senses, potewa na akili, rushwa na akili, simia roho, fathaika*. Recover the senses, *jirudia, pata akili tena*. Common sense, *waonavyo watu wote, akili ya watu wote, akili za kadiri ya binadamu*. It is a matter of common sense, *killa mtu husema hivi, inakubalika na wote*. Moral sense, *kupambanua mema na mbaya*.

Senseless, a. -*jinga, -pumbafu, pasipo akili*. Be (become) senseless, *simia roho*.

Senselessness, n. *ukosefu wa akili, upumbafu*.

Sensibility, n. (sense) *akili*; (sensitivity) *wepesi wa kuona, kustuka upesi*.

Sensible, a. (prudent) -*enyi akili, -a busara, -a maana*; (palpable, perceivable) [-*a kuoneka na Senses*]. Be sensible of, *ona, jua, tambua*. He is sensible, *akili zake anazo*; (conscious) *amejirudia*.

Sensitive, a. -*epesi kuona* [*kustuka, kubadilika, kugeuka, kuwa na hasira ao chuki, &c.*], -*siovumilia maumivu*. The sensitive plant, *kifa uwongo*.

Sensitiveness, n. [*hali ya kuwa Sensitive*].

Sensual, a. -*a mwili, -a mambo ya mwili, -a furaha za mwili, -a tamaa za mwili*; (licentious) -*a anasa, -a ufisadi, -asherati, -a ngoa*.

Sensualism, n. = **Sensationalism**; = **Sensuality**.

Sensualist, n. *mtu wa Sensualism*.

Sensuality, n. *kuwa Sensual*.

Sensualize, v. *haribu kwa anasa za mwili, ongoza vibaya, geuza kinyama*.

Sensuous, a. = **Sensual**; -*a Senses*.
Sent, p. t. na pf. t. ya Send.

Sentence, n. (verdict) *hukumu, maamuzi, neno la kathi*; (decision) *shauri, wosia*; (maxim) *mfano wa maneno, mithali*; (in grammar) [*fungu la maneno lenyi kupasha habari*].

— **v.** (give, pronounce sentence on) *pasisha athabu, hukumu, amua, kata hukumu*. He has been sentenced to death, *amekatiwa hukumu ya kuuawa*.

Sententious, a. -*enyi maneno ya hekima, -a kujivuna* [*kwa kuwa na maneno ya hekima*], -*a kujifanya mwalimu*.

Sentient, a. -*enyi akili ya kuona* [*si kama mmea, ao jiwe*].

Sentiment, n. *nia, shauri* [*ma-*], *neni* [*ma-*].

Sentimental, a. -*enyi Sentimentality, -otaji*.

Sentimentalist, n. *mtu wa Sentimentality*.

Sentimentality, Sentimentalism, n. *kuotaota, kujitungia mawazo moyoni, kuchukuliwa na fikara, wepesi wa kuvutwa na tamaa*.

Sentinel, Sentry, n. *asikari, mngoje* [*wa-*] *zamu, mlinsi, mvizia*.

Sentry-box, n. *kituo* [*kibanda*] *cha Sentry*.

Separable, a. -*a kutengeka, -a kubaguka*.

Separate, a. *mbali, -liotengwa, peke yake* [*yao, &c.*], -*moja-moja*.

— **v.** *tenga, gawa, weka mbali, farikisha, bagua, changanua*.

Separation, n. *mtengano, kuachana, mgawo, kufarakana, kuwa mbali, kuwa peke yake* [*yao, &c.*].

Separatism, n. [*kutengana na Kanisa la kimasihya*].

Separatist, n. *mtu wa Separatism*.

Sepoy, n. [*asikari wa kihindi*].

September, n. [*mwezi wa kenda kisungu*].

- Septennial**, a. -a miaka saba, -a killa mwaka wa saba.
- Septic**, a. -a kuozesha.
- Septuagenarian**, n. [mtu wa miaka sabwini umri wake].
- Septuagesima**, n. [juma a pili ya tatu mbele ya mwanzo wa Lent].
- Septuagint**, n. [maandiko matakatifu ya Wayahudi yamefasirika kwa kiyonani, Agano la kale kwa kiyonani].
- Sepulchral**, a. -a kaburi; (of sound) -a kulia wazi, -a sauti nene.
- Sepulchre**, n. kaburi [ma-], ziara [ma-].
- Sepulture**, n. kuzika, maziko.
- Sequel**, n. mwisho, mambo ya baadaye.
- Sequence**, n. mwandamano, ufuatano, utaratibu.
- Sequester**, v. twaa [mali ya mtu kwa muda fullani], shika rahani, weka; (separate) weka mbali, tenga.
- Sequestered**, a. -a faragha, -a mbali, pasipo watu, ukiwa.
- Sequesterate**, v. = Sequester.
- Sequestration**, n. kutwaa [kutwaliwa] mali (Taz. Sequester).
- Sequestrator**, n. [afanyaye Sequestration].
- Seraglio**, n. [nyumba ya waanake wanapotengwa], harimu.
- Seraph**, n. [malaiika].
- Seraphic**, a. -a Seraph.
- Serenade**, n. [kwimba nyimbo ao kupiga ngoma usiku za kumsalimia mchumba na kumwita, nyimbo ao ngoma ya usiku].
- Serene**, a. -eupe, safi, -kunjufu, -tulivu.
- Serenity**, n. weupe, ukunjufu, utulivu; (of weather) kweupe, kutakata.
- Serf**, n. mtumwa [wa-].
- Serfdom**, n. utumwa.
- Serge**, n. [nguo kama Cloth].
- Sergeant**, n. [msimamizi wa asikari, sajin].
- Serial**, a. [-a kutokea marra kwa marra kwa muda wake].
- Series**, n. mafuatano, mwandamano, safu, ufululizo.
- Serious**, a. (grave) -siocheka, -zito, -a kuonya; (important) -a maana, enyi habari kubwa [nzito], -kubwa. A serious offence, kosa kubwa.
- Seriously**, adv. kwa kuonya; (very) sana.
- Seriousness**, n. uzito, &c. (Taz. Serious).
- Sermon**, n. hotuba, mahubiri ya anjili, maneno ya kuonya.
- Sermonize**, v. onya onya, chosha kwa maonyo, hubiri ovyo.
- Serous**, a. -a mtindi, kama mtindi.
- Serpent**, n. nyoka mkubwa.
- Serpentine**, a. -enyi mapindi, -a kuzingamana, -a kuzunguka, -a kupindikapindika.
- Serrated**, a. -lio chongoka, kama msumeno.
- Serried**, a. -a kusongana, -a kusongwa.
- Serum**, n. mtindi.
- Servant**, n. mtumishi [wa-], mtumwa [wa-], hadimu [ma-]; (female) mjakazi [wa-]; (girl) kijakazi [vi-]; (European's household) boi [ma-].
- Serve**, v. tumikia, hudumia, ngojea, tendea kazi, -wa mtumishi; (be of use) faa; (treat) tendea; (give out) toa. Serve out, toa; (have revenge on) lipiza kisasi. Serve up, pakua, andalia, andika. Serve for, faa mahali pa. I will serve you out, nitakulipa. It serves you right, astahili yako. He has served his time, amemaliza kazi yake, amewadi.
- Server**, n. mngoje, mngojezi.
- Service**, n. utumwa, hudumu, utumishi, kazi; (use, employment) matumizi, mafaa; (help) fathili, msaa, shime; (of china, &c.) jamii [ya vyombo vya kulia]; (worship) sala ya dini, ibada, hitima, fathiha; (= Army, ao Navy). Divine Service, ibada, dini. He is on service, yuko katika kazi yake. See service, tumika ritani.

Serviceable (Be), a. *faa, -wa -a kufaa, tumika, -wa -zima.*

Servile, a. *-a kitumwa, -nyonge, -baya*; (literal) *-a kufuasa maneno mno.*

Servility, n. *unyonge, kufanya kitumwa, kushika miguu.*

Servitor, n. *mtumishi [wa-], mfuasi [wa-].*

Servitude, n. *utumwa.*

Session, n. *baraza, muda wa kubarizi.* Hold a session, *barizi.*

Set, v. (p. t. na pf. t. **Set**); (place) *weka, tia mahali, tia*; (fix) *kaza*; (cause) *fanya*; (settle, order) *amrisha, agiza*; (razor, &c.) *noa*; (trap) *tega*; (sail) *tweka*; (in line) *panga*; (with jewels, &c.) *pamba*; (of sun) *-chwa, shuka*; (of fluids) *gandamiza*; (current) *enda, pita*; (plants) *panda*, (neut.) *toa mizizi, anza kuota*; (a fashion) *anzisha, sua*; (a timepiece) *kabilisha vema mikono [ya saa]*; (a broken bone, &c.) *unga, ungisha.* Set an example to, *fuasisha.* Set about, *shika kazi ya, anza, maliki.* Set apart, *weka mbali, tenga, bagua.* Set aside, *weka, acha, kataa, tangua.* Set at naught, *tharau, tweza, thihaki.* Set at ease, *tuliza, sterehisha, teremesha.* Set by, *weka.* Set store by, *tunuka.* Set down, *weka*; (a load) *tua, panga*; (humiliate) *tweza, thili*; (put down in writing) *andika.* Set eyes on, *tazama, tupia jicho.* Set forth, (explain) *eleza, tangaza*; (neut.) *shika njia, ondoka.* Set forward, *endelea*; *himiza, endesha.* Set in (rain), *anza shika.* Set going, Set on foot, *endesha, anzisha.* Set on, (attack) *shambulua, rukia*; (urge to fight) *piganisha, chomeshu.* Set off, *pamba, tia urembo, chukua*; (separate) *tenga*; (neut.) *ondoka, funga safari.* Set on fire, *choma, tia moto, washa*; (put on the fire) *teleka.* Set out, *andika, rakibisha, weka vizuri*; (neut.) *ondoka, shika njia.* Set right,

tengeneza, fanyiza. Set side by side, *ambazana, pambanisha, weka kando kando.* Set teeth on edge, *tia ganzi la meno.* Set to, *tia katika*; (neut.) *shika kazi*; (fight) *pigana.* Set to work, *-pakazi*; (neut.) *shika kazi.* Set to music, *fanyizia [maneno] uimbo, linganisha sauti [ya ngoma, kinanda, &c.].* Set up, (upright) *simamisha*; (business) *anza [ingia, shika], kazi [shughuli]*; (pretend) *jifanya*; (in type) *panga vichapa.* Set upon, *endea kwa nguvu, shambulua.* Set going, *endesha.* Set thinking, *fikirisha, tia fikarani.*

Set, a. (appointed) *-liokazwa, -liokamriwa, -a lazimu*; (firm, fixed) *thabiti, -gumu, -siogeuka.* A set speech, *maneno ya utaratibu.*

— n. *jamii*; (of a current) *mvuto, mkondo*; (form) *namna, hali*; (friends, relatives, &c.) *jamaa, utani.* Make a set (dead set) at, *endea, jaribia sana.*

Set-off, n. *malipizi, sawa, kisasi.*

Settee, n. *kiti kirefu, kitanda [vi-].*

Setter, n. *[mbwa wa kuwinda].*

Setting, n. *kuweka, &c. (Tax. Set, v.); (of sun) kuchwa, mshuko*; (of a jewel, &c.) *kijalizo.*

Settle, v. (fix) *kaza, fanya imara, weka thabiti*; (quiet) *tuliza, sterehisha*; (decide) *hukumu, kata jambo [neni], amua, maliza*; (make clear, show) *onyesha, thihi-risha, eleza, thubutisha*; (adjust) *tengeneza, patanisha*; (accounts) *fanya safi [barabara], lipa [deni]*; (colonize) *kalisha watu katika*; (reside) *kaa*; (rest) *tua, tulia*; (sink down) *titia, shuka*; (get clear) *tuama*; (resolve on) *yakinia, azimu, nia.*

Settled, a. *imara, thabiti, -tulivu, makini.* Settled resentment, *makamio, mfundo.* A settled country, *[inchi inayokoa watu kwa amani, inchi yenyi amani].*

Settlement, n. *kukaza, &c. (Tax. Settle); [makazi ya watu waliyo-*

- hamia*], *mji mpya, kikao*; (inheritance) *urithi, wosia, mali iliyorithiwa*; (agreement) *mapatano*.
- Settler**, n. *mhamia mahali, mgeni, mjaji, mja na maji*; (final step) *mwisho*. That's a settler, *bass, imekwisha*.
- Seven**, n. *na a. saba, sabaa*.
- Sevenfold**, a. *-a marra saba*.
- Seventeen**, a. *na n. sabatashara*.
- Seventh**, a. *-a saba*.
- Seventy**, a. *na n. sabwini*.
- Sever**, v. *kata, tenga, vunja*.
- Several**, a. *-ingine, -ingi kidogo, si -ingi, baathi, kathawakatha*; (some people) *watu*; (separate) *-moja moja, killa -moja*.
- Severally**, adv. *mojamoja, killa mtu*.
- Severance**, n. *kukata, kutenga*.
- Severe**, a. *-kali, zito, -a nguvu*.
- Severity**, n. *ukali, &c.*
- Sew**, v. (pf. t. **Sewed, Sewn**) *shona*.
- Sewage**, n. *takataka, mavi, matakato*.
- Sewer**, n. *mshoni [wa-]*; (drain) *mfereji [mi-, wa kuchuruzisha taka mavi, &c.]*.
- Sewing**, n. *ushoni*.
- Sewn**, pf. t. *ya Sew*.
- Sex**, n. [*hali ya kuwa kiume ao kike*].
Male sex, *waanaume, watu wa kiume*. Female sex, *waanake, watu wa kike*.
- Sexagenarian**, n. [*mtu wa miaka settini umri wake*].
- Sexagesima**, n. [*juma a pili ya pili mbele ya mwanzo wa Lent*].
- Sexennial**, a. *-a miaka sita, -a killa mwaka wa sita*.
- Sext**, n. [*sala za aththuuri*].
- Sextant**, n. [*chombo ao kipande cha kupimia urefu kwa pembe (angles)*].
- Sexton**, n. [*mngoje wa mlango wa kanisa, mtunza kanisa, mlinzi wa kanisa, mtunza kanisa, mlinzi wa makaburi, mzishi*].
- Sexual**, a. *-a Sex, -a kiume kuliko kike, -a kike kuliko kiume*. Sexual passion, *ng'oa*. Sexual organs, (male) *mboo [mi-], ume*, (female) *kuma, uke*.
- Sexuality**, n. *kuwa na Sex*.
- Shabbiness**, n. *ukukuu, unyonge, &c.*
- Shabby**, a. *-kukuu, -baya, -liocharaa*; (mean) *-nyonge, -a choyo*.
- Shackles**, n. *pingu*.
- Shaddock**, n. *furungu [ma-]*.
- Shade**, v. *tia kivuli, kinga jua*; (protect) *tunza, funika*.
- , **Shadow**, n. *uvuli, kivuli [vi-]*; (darkness) *giza*; (variation) *tofauti ndogo*; (protection) *hamaya, uinzi*; (likeness) *mfano*; (of a lamp) *chengeu, kisetiri*. A shade of difference, *tofauti ndogo*. Shade of colour, *rangi, ginsi ya rangi*. Shade of meaning, *maana, kionyo*. Sun shade, *mwavuli [mi-]*.
- Shadow**, v. *tia kivuli, tia giza*; (describe dimly) *eleza kidogo*.
- Shadowy**, a. *-a kivuli*; (vague) *si yakini, si hakika, si halisi*.
- Shady**, a. *-a Shade, -enyi Shade*; (mean) *-nyonge, -baya*.
- Shaft**, n. [*kitu cho chote kilicho kirefu na chembamba, kama mwanzizi*]; (wooden part) *uti, mti*; (of arrow) *wano [ma-]*; (missile) *mshale [mi-], mkuki [mi-]*; (pit) *shimo [ma-], tundu [ma-]*; (chimney) *dohani*; (of metal) *ufito [wa chuma, &c.]*.
- Shaggy**, a. *-enyi nyele nyingi za msokoto, -a manyoya ya msongo*.
- Shagreen**, n. [*ngosi iliyotengenezwa ya frasi, kondoo, &c.*].
- Shah**, n. *Sultani wa Ajjemi*.
- Shake**, v. (p. t. **Shook**, pt. t. **Shaken**) *tikisa, tetemesha, sukasuka*; (neut.) *tikisika, tetemeka*; (weaken) *thoo-fisha, punguzia nguvu, ondolea uthabiti, tia mashaka*. Shake off (fruit), *pukusa*. Shake hands, *pana mkono, shikana mikono, amkiana*. Shake out, *futua, kunguta, kupua*.
- n. *kutikisika, &c., mtikiso, tetemo [ma-], tetemeko [ma-], msukosuko*. Hand-shake, *kitetemeshi*.
- Shako**, n. [*kofia ya asikari*].
- Shaky**, a. *-a kutikisika, &c. (Taz. Shake, v.)*; (weak) *thaiifu*.
- Shale**, n. [*mawe kama matope yaliyokauka sana*].

Shall, v. (p. t. **Should**), (in verbs) *-ta-*. I shall go, *nitakwenda, nenda*. You shall go, *huna buddi kwenda, nenda*. Shall I go? *niende?* Shall you go? *unakwenda?* You shall not go, *huendi, usiende*. If you go, I shall, *ukienda nitakwenda*.

Shallow, a. (of water) *-chache, haba, kidogo*; (foolish) *-a akii chache, -pumbafu*.

Shallowness, n. *kuwa Shallow*.

Shaly, a. *-a Shale*.

Sham, n. *kujifanya, mwigo, mfano mtupu*; (hypocrisy) *unafiki, uwongo*.

— a. *-a Sham*. Sham fight, *kucheza vita*.

— v. *jifanya, jigeusa*. Shamming dead, *kufa uwongo*. Sham sickness, *jigonjweza*.

Shambles, n. *matindo, mahali pa kuchinja nyama*.

Shame, n. (disgrace) *aibu, fetheha*; (modesty) *haya*.

— v. *tia haya, aibisha, fethehesha*.

Shamefaced, a. *-enyi haya nyingi*.

Shamefacedness, n. *kuwa Shamefaced*.

Shameful, a. *-a kutia haya, -a kuaibisha, -a kufethehesha, -baya sana*.

Shameless, a. *-pujufu, -pofu wa haya, pasipo haya*. Lead a shameless life, Act shamelessly, *jipujua*.

Shamelessness, n. *kuwa Shameless*.

Shampoo, v. *kanda [mwili, maungo], osha kitwa na nyele*.

Shamrock, n. [*ua la Ireland na ishara yake*].

Shank, n. [*kipande kirefu cha kati*]; (of leg) *mguu [toka goti kwa chini]*.

Shanty, n. *kibanda, kipenu [vi-]*.

Shape, n. *umbo, namna, sura, mfano*. Take shape, *onekana, pata umbo*.

— v. (fashion) *fanyiza, tengeneza*; (direct) *ongoza, elekeza*.

Shapeless, a. *pasipo uzuri, -a vivi hivi, -baya*.

Shapelessness, n. *kuwa Shapeless*.

Shapeliness, n. *uzuri [wa umbo]*.

Shapely, a. *-suri, -a namna*.

Share, v. (divide) *gawa, gawanya*; (partake of) *shariki*.

— n. *fungu [ma-], sehemu, nussu*; (part of capital) [*fungu la ras il mali ya Company*]; (of plough) [*chuma cha jembe la kulima kwa ng'ombe*]. Have shares in, *-wa mshiriki wa*. Go shares in, *shariki, sharikiana*.

Shareholder, n. [*mshiriki mali ya Company*].

Sharer, n. *mshiriki [wa-]*.

Shark, n. *papa*; (rogue, sharper) *ayari, mjanja [wa-]*.

Sharp, a. *-kali, -enyi ncha, -liocho ngoka*; (vigorous, clever) *-enyiakili, hodari, -erevu, bingwa, -a nguvu, -epesi*; (in dealing) *-erevu, -janja, -danganyifu, kalam'zi*; (quick) *-epesi kuona, -ekevu, hodari*; (bitter) *-chungu, -kali*; (shrill) *-embamba*; (thin) *-embamba, -liokonda, -liogeuka kwa njaa*. A sharp turn, *kugeuka upesi, pindi la marra moja*. Sharp practice, *hila, ujanja, udanganyifu*. Look sharp! *haya! upesi! hima!*

— n. (in music) [*sauti iliyokarwa kidogo; alama yake*].

Sharpen, v. (edge) *noa, tia makali*; (point) *chonga, chongoa, fanya -kali*; (arouse) *amsha, tia bidii*.

Sharper, n. *ayari, mjanja [wa-], kalam'zi*.

Sharpness, n. *ukali, uchungu, &c. (Tax. Sharp, a.)*.

Sharp-shooter, n. *mwenyi shebaha*.

Sharp-sighted, a. *-a kutazama mbali, -enyi macho ya nguvu, macho*.

Sharp-witted, a. *-a akili, -a busara*.

Shatter, v. *vunjavunja, pondaponda, haribu kabisa, pasua*.

Shave, v. (pf. t. **Shaved, Shaven**) *nyoa [kitwa]*; (smooth) *lainisha [mti kwa kisu]*; (pass close to) *pita karibu ya, ambaa*.

Shaving, n. (of wood) *takataka za mbau, masafi*; (of hair) *kunyoa, unyozi*.

Shawl, n. *shali*; (waist) *mahazamu*.

She, pron. *yeye [mwanamke], yule*,

- huyo*; (in verbs) *a-*. *She-*, *-a kike*, *jike*.
- Sheaf**, n. (pl. **Sheaves**), (of cut rice, &c.) *mganda* [*mi-*].
- Shear**, v. (pf. t. **Sheared**, **Shorn**) *kata*, *kata manyoya*, *nyoa*.
Stoutness, n. *unene, nguvu, uthabiti, maki*; (of limb) *maungo*.

Stove, n. *jiko [meko, la kizungu, chombo chenye moto cha kupikia]*.

— p. t. *ya Stave, v*.

Stow, v. *weka, pakia, tia vizuri*.

Stowage, n. *mapakizi, nafasi ya kupakilia vitu*.

Straddle, v. *tagaa, panua miguu*.

Straggle, v. *tawanyika, tapakaa, enea*; (be behindhand, be lost) *chelewa, potea*.

Straggler, n. *aliyepotea, mpotefu wa njia, mchelewa*.

Stragglings, a. -*liotawanyika -liotapakaa*; (late) -*liochelewa*.

Straight, a. *sawa, -a kunyoka, -a kusimama*; (honest) -*nyofu, amini, halisi*. Go straight on, *endelea moja kwa moja*.

Straighten, v. *nyosha, fanya sawa, tengeneza*; (put in difficulties) *uthi, thiikisha*. Straightened circumstances, *uthiiki, ukwasefu*.

Straightforward, a. -a *kwenda sawa*; (honest) -*nyofu, amini*.

Straightness, n. *kuwa Straight*.

Straightway, adv. *marra moja, palepale, ghafala hiyo*.

Strain, v. *vuta kwa nguvu, nyosha, kaza*; (make effort) *jitahidi, fanya bidii, kakamuka*; (over-exert, sprain) *stusha, tegua, popotoa, legeza*; (liquid) *chuja*; (meaning) *geusa, haribu*; (principles, point) *kosea kidogo makusudi, vuta*.

— n. (exertion) *juhudi, bidii, kakamuka*; (stretching) *kunyoshwa*

- sana, mkazo*; (of music) *uimbo, sauti*; (manner) *ginsi, mfano*; (natural bent) *katiba, tabia*.
- Strained, a.** -a *shidda, -a mashaka, -a baridi*.
- Strainer, n.** (wicker) *kung'uto [ma-], kifumbu [vi-]*.
- Strait, a.** -*embamba, -a mkazo*; (rigid, stern) -a *shidda, -kali*.
- , **Straits, n.** (of sea) *kilango cha bahari, mlango*; (distress) *shidda, taabu*. Be in straits, Be put to straits, *kwama, thiiki pata mashaka*.
- Straiten, v.** *songa, kaza, ongezea taabu*.
- Strait-laced, a.** -*gumu, -shupafu*.
- Straitness, n.** *shidda, taabu*.
- Strait-waistcoat, n.** [*vazi nene zito la kufungia walevi, wenyi wasimo &c.*].
- Strand, n.** *ufuko, ukingo wa bahari*; (in rope) *jino la kamba, ncha*. A rope of three strands, *kamba ya meno matatu*.
- v. *pweleza, ingiza [ingia] mwambani, kwama, kwamisha*.
- Strange, a.** -*geni, -zungu, ajabu, -pya, -a uzushi*; (belonging to another) -a *watu, -a mwenyewe*.
- Stranger, n.** *mgeni [wa-]*. He is a stranger to me, *simjui huyu*. You are a stranger (rare visitor) nowadays, *umeghalika siku hizi*.
- Strangle, v.** *nyonga, songa kwa kamba*; (throttle) *kaba, kaba roho*; (put a stop to) *komesha, suia*.
- Strangulated, a.** -*liosongwa*.
- Strangulation, n.** *msongo wa mshipi, msongo wa roho*; (strangling) *kusonga kwa kamba, kunyonga*.
- Strap, n.** *ukanda [kanda]*.
- v. *funga [piga] kwa Strap*.
- Strata, pl.** *ya Stratum*.
- Stratagem, n.** *hila, werevu*.
- Strategic, a.** -a **Strategy**.
- Strategist, n.** *mwenyi maarifa ya vita*.
- Strategy, n.** *maarifa ya vita, mate-ngeneo [madaraka] ya vita*.
- Stratification, n.** *kufanya Stratum, ginsi ya Stratum*.
- Stratify, v.** *fanya Stratum*.
- Stratum, n.** [*mawe ya kuwekwa safu safu, ya kupangilika juu kwa juu, ya tabaka, ya kutabikiana, ya kulaliana, ya kutandwa sawa sawa, matandiko ya mawe*], *tabaka [ma-]*.
- Straw, n.** *majani makavu [ya ngano, ya shayiri]*; (trifle) *si kitu, robo pesa*. The last straw, [*kitu kidogo kiletacho maangamizi makuu, chenyi hasara kubwa*]. It does not matter a straw, *haithuru hatta kidogo*.
- Strawberry, n.** [*tunda tamu la kisungu*].
- Stray, v.** *potea, sungukazunguka*; (err) *kosa*.
- a. -*liopotea*; (chance) -a *bahati, -a vivi hivi, -a nasibu*.
- Streak, n.** *mfuo [mi-]*; (of light) *kianga*.
- v. *piga mifuo*.
- Streaky, a.** -*enyi mifuo*.
- Stream, v.** *pita [kama maji ao mwannga], pita tele*. Go up stream, *kata maji*. Go down stream, *fuata maji*.
- n. *mto mdogo [mi-], kijito [vi-]*; (current) *mkondo*; (tendency) *maelekeo, mvuto*.
- Streamer, n.** *bendera [ndefu nyembamba]*.
- Streamlet, n.** *kijito [vi-]*.
- Street, n.** *njia ya mji*.
- Strength, n.** *nguvu, uwezo, sulubu, uthabiti, ugumu*. On the strength of, *kwa kutegemea, kwa sababu ya*.
- Strengthen, v.** *tia nguvu, fanya imara, thubutisha*; (encourage, help) -*pa moyo, sayidia, fariji*.
- Strenuous, a.** -a *bidii, -a nguvu, -a kujitahidi*.
- Stress, n.** (trouble) *shidda*; (strain) *mkazo, kusonga*; (means, force) *maana, nguvu*. Lay stress on, *ona -kubwa*; (emphasize) *kazia sauti*. Stress of weather, *pepo nyingi, taabu ya bahari*.
- Stretch, v.** *nyosha, eneza, kunjua, tanda, tanua, wamba, (neut.) nyoka, tanuka, enea*; (exaggerate)

ongeza mno, pita kiasi ya, vuta.
 Stretch up to, *chuchumia*. Thing stretched over, *kiwambo*.
Stretcher, n. *kitanda* [*cha kuchukulia wagonjwa*], *machela*; (in boat) *wango* [*ma-, mb-*], *taruma* [*ma-*].
Strew, v. (pf. t. **Strewed**, **Strown**) *tawanya, tapanya, tupa huko na huko, mwaga, nyunyiza*.
Stricken, a. *-liojeruhi, -liotaabika, -enyi kupigwa*.
Strict, a. *halisi, -a nguvu, -kali*.
Strictness, n. *uhalisi, ukali, nguvu*.
Stricture, n. *shutumumu* [*ma-*], *neni* [*ma-*] *kali, suto* [*ma-*]; (medical) *kusongwa mshipa*.
Stride, v. (p. t. **Strode**, pf. t. **Stridden**) *panua miguu, tagaa, enda kwa mashindo, piga hatua ndefu, chapua miguu*.
 — n. *hatua kubwa, mwendo wa nguvu*. Advance by rapid strides, *endelea upesi*.
Strife, n. *shindano, ushindano*; (war) *vita, pigano, kondo*; (quarrel) *ugomvi, kubishana*.
Strike, v. (p. t. *na* pf. t. **Struck**) *piga, chapa*; (knock) *gonga. bisha, gota*; (with knife, &c.) *piga, choma*; (coin) *piga chapa*; (sail, &c.) *tua, shusha*; (on rock) *kwama, ingia mwambani*; (leave work) *acha kazi* [*illi kuzidisha ijara*]; (affect) *ingia moyoni, stusha, shangaza, choma, tia kishindo*. It strikes me, *nathani, nia imeniingia moyoni*. He was struck by fever, *alipatwa na homa*.
 Strike a balance, *fanya urari wa hesabu, lipana, katiana*. Strike a bargain, *patana, pigana bei, fanya ubazazi*. Strike a camp, *vunja kituo, ondoka*. Strike a light, *washa taa*. Strike a tent, *ng'oa* [*ondoa*] *hema*. Strike off, *futa, kata, katia mbali*; (print) *piga chapa*; (diverge) *enda zake* [*sao, &c.*]. Strike out, *toa, futa*; (invent) *vumbua, jitungia, jifanyizia*. Strike up, (music) *anza, anza kuimba* [*kuchezza*]. Strike on, *kuta*; (discover)

vumbua. Strike on the ground, *tupa chini*. Strike in, *jitia gha-fala, jiingiza katika maneno*. Strike a sore place, *tonesha*.
Strike, n. [*kuacha kazi illi kuzidisha ijara, makatazo ya kazi*].
Striking, a. *-a kustusha* [*kushangaza, kustaaajabisha, kushinda moyo, &c.*]. The effect was most striking, *mwisho wake ajabu sana*.
String, n. *kitani, uzi, ugwe, kigwe*; (of fibre, &c.) *upote* [*pote*]; (series) *wingi moja kwa moja, mwanda-mano, mfuatano*; (row) *safu*; (of beads) *shada*; (of fish) *mtungo* [*mi-*].
 — v. (p. t. *na* pf. t. **Strung**) *fungia kitani, tunga*.
String-course, n. *ushi* [*ny-*].
Stringed, a. *-enyi nyuzi*.
Stringency, n. *nguvu, ukali, mkazo*.
Stringent, a. *-a nguvu, &c.*
Stringy, a. *kama nyuzi, kama kitani*.
Strip, n. *kipande* [*kirefu chembamba*]. Strips of grass, or leaf, for making mats, brushes, &c., (fine) *myaa* [*mi-*], (coarse) *mwaa* [*miwaa*]. Plaited strips, (fine) *ukili* [*kili*], (coarse) *skupatu* [*ma-*], (coloured) *nyiza*. Strip of bark, fibre, &c., *upote* [*pote*], *ng'ong'e*.
 — v. (clothes) *vua, vulia*; (skin) *chuna*; (property) *kumba, nyang'anya, teka, fanya -tupu* [*kame*]; (rind, &c.) *ambua, babua*; (leaves, &c.) *ponoa, pagua*; (thatch) *ezua*; (branches, &c.) *kwanua*.
Stripe, n. (line) *utepe* [*tepe*], *uzi* [*ny-*], *mfuo* [*mi-*], *mwalamu* [*mi-*], *mlia* [*mi-*]; (blow) *pigo* [*ma-*].
Striped, a. *-a mistari, -a tepe, -a milia*.
Stripling, n. *kijana, pande la mwana*.
Strive, v. (p. t. **Strove**, pf. t. **Striven**) *jaribu, jaribia, jitahidi, fanya bidii, shindana*.
Strode, p. t. *ya* **Stride**, v.
Stroke, v. *papasa*.
 — n. *pigo* [*ma-*]; (disaster) *msiba* [*mi-*], *athabu*; (sudden effort or

- effect) *tendo la nguvu, tendo kubwa, mshindo, tharuba*. Give a finishing stroke to, *maliza, kamilisha*. At a stroke, *tharuba moja*.
- Stroll**, v. *zungukazunguka, tembea-tembea, tanga, jienda*.
- n. *matembezi, kuzunguka, kutanga*.
- Stroller**, n. *mpitaji, mtembezi*.
- Strong**, a. -a *nguvu, hodari, ndume, -a bidii, thabiti, sulubu, imara, -gumu*.
- Stronghold**, n. *ngome, boma [ma-], gereza*.
- Strongly**, adv. *kwa nguvu, sana*.
- Strop**, n. *kinoo cha wembe*.
- Strophe**, n. *sehemu ya uimbo*.
- Strove**, p. t. ya **Strive**.
- Struck**, p. t. na pf. t. ya **Strike**, v.
- Structural**, a. -a **Structure**.
- Structure**, n. *muundo, ujenzi, mate-ngeneo*; (natural form) *umbo, ginsi ya kufanyizwa, maumbile, asili*. A structure (building), *jengo [ma-]*; (wooden) *kiunzi [vi-]*.
- Struggle**, v. *shindana, jitahidi, toa bidii, jaribu, jaribia, tapatapa, kakamuka*.
- n. *bidii, mkazo, jaribu [ma-], juhudi, kazi ngumu*; (contest) *shindano, mapigano, vita*.
- Strung**, p. t. na pf. t. ya **String**, v.
- Strut**, v. *tamba, enda kwa kujivuna, enda kwa umalidadi*.
- n. *kutamba, &c.*; (cross-piece) *taruma [ma-]*.
- Strychnia**, n. [*sumu ya mtonga ao mtupa*].
- Stubble**, n. [*mashina ya majani ao ya mabua yaliyokatika*].
- Stubborn**, a. -*tundu, -shupafu, -kaidi, -gumu*.
- Stubby**, a. (hair) -*fupi na -nene*.
- Stucco**, n. *chokaa ya kukandika*.
- Stuck**, p. t. na pf. t. ya **Stick**, v.
- Stud**, n. *jamii ya frasi [waliochungwa kusudi kuzaliana]*; (button) *msomari, kifungo, kinundu*.
- v. *pamba kwa vinundu, tapakaa katika*.
- Student**, n. *mwanafunzi, mwana*
- chuoni, mtu wa kusoma, mtu wa mtaala*.
- Studied**, a. (designed) -a *bidii, -a makusudi*; (worked at) -*liofanyiwa kazi nyingi, -liosomwa sana*.
- Studio**, n. [*kiwanda cha mfanyi sanamu*].
- Studious**, a. -a **Study**, n.
- Studiousness**, n. *bidii ya kusoma*.
- Study**, n. (mental work) *kujifunza, kusoma kwa bidii, mtaala*; (subjects studied) *kazi za chuoni, vitabu, masomo, kazi*; (in art) *kazi, namna ya kazi, -kielezo*; (room) *kijumba cha kusomea*.
- v. *soma, soma sana, jifunga kwa kusoma, fanyia bidii, taali*.
- Stuff**, n. *vitu, vyombo, vifaa, vipambo vya nyumba*; (cloth) *nguo*; (nonsense) *takataka, upuzi, mawe, ovyo*; (substance) *asili, kitu cha asili, kitu*.
- v. *jaza, jaliza*; (press) *shindilia, songeza*; (gorge) *shibisha, vimbisha, kinaisha*; (fill hole) *ziba*; (cram with learning) *fundisha mambo mengi mno*.
- Stuffing**, n. [*maandasi ya kukolea chakula; kitambaa cha kuzibia*].
- Stuffy**, a. *pasipopita hewa, -a jasho, -a kusonga*.
- Stultification**, n. *kupumbaza*.
- Stultify**, v. *pumbaza, -onya upumbafu wa*; (disappoint) *batilisha, tangua, vunja*.
- Stumble**, n. *kwao [ma-]*; (error) *kosa [ma-]*.
- v. *jikwaa, kwaa*. Stumble upon, *kuta, pata kwa bahati, bahatisha*.
- Stumbling-block**, n. *kikwazi, jambo la kukosha, mtu wa kuchukiza, mashaka*.
- Stump**, n. [*kipande cha mti kilichobaki*], *shina [ma-], konyo [ma-], shiku, kishiku*; (limb) *gutu, kigutu*; (of arm) *kikono*; (in cricket) [*mti (mi-), kiguzo (vi-)*]. Go on the stump, *zunguka na hubiri*. Draw stumps (in cricket), *vunja [mchezo], maliza*.

- Stump**, v. (walk heavily) *enda kwa kukanyaga, jikokota*; (in cricket, put out) *funga*; (tour in) *zunguka na hubiri katika*.
- Stumpy**, a. Be stumpy, *kundaa, vin*.
- Stun**, v. (bewilder) *fathaisha, tia bumbuazi, tisha, stusha*; (with noise) *ziba masikio, tia kiziwi, levya*.
- Stunk**, pf. t. ya **Stink**, v.
- Stunt**, v. *viza, fupisha, haribu*. Be stunted, *via, kundaa, si kua vema*.
- Stupefaction**, n. *fathaa, bumbuazi, kupotewa akili*.
- Stupefy**, v. *tia Stupefaction*.
- Stupendous**, a. *-kubwa [-ingi] mno ajabu*.
- Stupid**, a. *-pumbavu, -jinga, pasipo akili*. You stupid! Stupid fool! *mbuzi wee! ng'ombe! ngamia!*
- Stupidity, Stupidness**, n. *upumba-fu, ujinga, akili chache*.
- Sturdily**, adv. *kwa nguvu, hodari*.
- Sturdiness**, n. *unene, nguvu*.
- Sturdy**, a. *-nene, -a nguvu, hodari*.
- Sturgeon**, n. [*samaki kubwa lenyi magamba*].
- Stutter**, v. *gugumiza, goteza maneno, babaika*.
- , **Stuttering**, n. *kigugumizi*.
- Sty**, n. (in eye) *chokea*; (for pigs) *banda la nguruwe, zizi [ma-]*.
- Style**, n. (kind) *ginsi, namna*; (appearance) *sura, umbo*; (good kind) *ginsi bora, namna nzuri*; (mode of writing) *andiko*; (temper) *tabia, desturi*; (title) *jina [ma-]*. A good (literary) style, *dibaji, ufasaha*. In style, *vizuri, kwa fahari*.
- v. *taja, ita*.
- Stylish**, a. *-zuri, bora*.
- Stylographic**, a. (pen) [*kalamu ya sindano na wino ndani*].
- Styptic**, a. *-a kuviliza damu*.
- Suasion**, n. *kushawishi, ushaushi*.
- Suave**, a. *laini, -tamu, -a kujipendekeza*.
- Subaltern**, n. *akida mdogo*.
- Subaqueous**, a. *-a chini ya maji*.
- Subdivide**, v. *gawa tena [zilio kwisha gawika]*, *zidi kugawa*.
- Subdivision**, n. *sehemu ya sehemu, kikato [vi-]*.
- Subdue**, v. *tiisha, piga, shinda*; (tame, quiet) *fuga, lainisha, tuliza*.
- Sub-editor**, n. [**Editor mdogo**].
- Subjacent**, a. *-a chini*.
- Subject**, n. [*kitu kinachonenwa au kutendewa kazi*]; (matter) *jambo, kitu, neno, shughuli*; (of king) *rayia*; (person) *mtu*.
- a. *-a chini*; (liable, affected) *-a kupaswa, -enyi kupasiwa, -lio katika hatari ya, -liopatikana na*.
- Subject to**, *kwa ruksa ya, kwa sharti ya*. He is subject to fits, *hupatika na kifafa*. Subject to your pleasure, *lakini upendavyo wewe*.
- v. *tiisha, weka chini*; (make liable, affect) *pasisha, pasha*.
- Subjection**, n. *utumwa, hali ya kuwa chini*.
- Subjective**, a. (things) *-a nafsi, -a nafsini [-a rohani, -a moyoni, -a akili, -a mawazo, -a kutungika moyoni tu, si halisi, si hakika]*; (person) *-a kujikumuka nafsi, -enyi fikara zake*.
- Subjectivity**, n. *kuwa Subjective*.
- Subjoin**, v. *tia mwishoni, ongeza, tia zayidi*.
- Subjugate**, v. *tiisha, piga, shinda*.
- Subjugation**, n. *kutiisha, kutiishwa, &c.*
- Subjunctive**, a. [**Subjunctive Mood, namna ya Verb yenyi kuonyesha wazo la moyoni (kusudi, tamaa, tumaini, hofu, &c.), si hakika ya jambo lenyewe**].
- Sublet**, v. [*pangisha nyumba, &c., iliopangwa*].
- Sublimate**, v. (turn to vapour) *geuza hewa kwa kutia moto*; (refine) *safisha kwa moto, takasa*.
- Sublimation**, n. *kugeuza, &c. (Taz. Sublimate)*.
- Sublime**, a. *-a juu sana, bora sana, -kuu, -tukufu mno, -a fahari, -a heri, ajabu*.
- Sublimity**, n. *fahari, heri, utukufu, ajabu (Taz. Sublime)*.

Sublunary, a. -a dunia hii, -a uli-mwengu; (unimportant) -nyonge, hafifu.

Submarine, a. -a chini ya bahari.

Submerge, v. tosa, zamisha chini, didimisha.

Submergence, **Submersion**, n. kutota, kutosha chini.

Submission, n. kushika miguu, kujitoa, utii; (meekness) uvumilivu, urathi, upole.

Submissive, a. -tii, -pole, -nyonge.

Submissiveness, n. kuwa Submissive.

Submit, v. (surrender) shika miguu, jitoa, jiweka chini, tii; (endure) vumilia, stahimili; (acquiesce) kubali, ona rathi; (put forward) toa, weka.

Subordinate, a. -a chini, -dogo.
— v. weka chini.

Subordination, n. kuweka [kuwekwa, kujiweka] chini; (obedience) utii, utaratibu.

Suborn, v. [tumia kuwa mashahidi ya uwongo], apisha uwongo.

Subpoena, n. [hati ya kulazimisha mtu kuja mbele ya kathi].
— v. tolea Subpoena.

Subscribe, v. toa fetha, changa mali; (sign) andika jina chini, tia usahihi; (support, approve) kubali, shuhudia, toa ithini.

Subscriber, n. mwenyi kuchanga, &c.

Subscription, n. (contribution) chango [ma-]; (approval) kukubali; (signature) kuandika jina, ithini.

Subsection, n. sehemu ya sehemu, kikato [vi-].

Subsequent, a. -a baadaye.

Subsequently, adv. baada, daadaye.

Subserve, v. faa, sayidia.

Subservience, n. kutii, kufaa.

Subservient, a. -a kutii, -a kufaa.

Subside, v. shuka, punguka, tulia; (water) -pwa; (masonry) titia.

Subsidence, n. kushuka, &c., kutitia.

Subsidiary, a. -a kusayidia, -dogo.

Subsidize, v. tolea fetha ya msaada.

Subsidy, n. fetha ya msaada.

Subsist, v. (exist, endure) -wa, kaa, ishi; (live) pata chakula, pona, lisha. Subsist on, -la, ponea, jilisha.

Subsistence, n. chakula, riziki, nafuu; (existence) asili, hakika, kuwamo.

Subsoil, n. udongo wa chini.

Substance, n. kitu, nyama, mwili; (matter) asili ya vitu vyote; (import) maana; (strength) nguvu, uthabiti; (wealth) mali, utajiri.

Substantial, a. (real) -a hakika, -a kweli; (strong) -a nguvu, thabiti; (wealthy) -a mali, -tajiri. A substantial (corporeal) ghost, kivuli chenye nyama.

Substantiate, v. thubutisha, hakikia, yakinisha, shuhudia.

Substantive, n. = Noun.
— a. -a hakika, -a kweli, -a nguvu.

Substitute, v. tia mahali pa -ngine, badilisha.
— n. badala.

Substitution, n. kutia [kutiwa] mahali pa -ngine, kubadilisha.

Substratum, n. [kitu kilicho ndani ao chini].

Substructure, n. [Structure ya chini, ujenzi wa chini, jukwaa].

Subtend, v. lekea, lekeana na, kabili.

Subterfuge, n. hila.

Subterranean, **Subterraneous**, a. -a chini ya inchi.

Subtle, **Subtile**, a. -janja, -erevu, -a hila nyingi; (delicate fabric) laini, -embamba, -zuri; (penetrating) -a kupambanua, -a akili, -a nguvu.

Subtlety, **Subtleness**, n. werevu, busara; (fineness) wembamba, ulaini; (force) akili, nguvu.

Subtract, v. toa, ondoa, twaa, chukua.

Subtraction, n. kuondoa, &c., kutwaa nussu; (in arithmetic) baki.

Suburb, n. kiunga [vi-].

Suburban, a. -a kiunga, kiungani.

Subvention, n. msaada.

Subversion, n. *kupindua*, &c. (*Taz. Subvert*).

Subversive, a. -a *kupindua*, &c. (*Taz. Subvert*).

Subvert, v. *pindua*, *angamiza*, *haribu*.

Succeed, v. (follow) *fuata*; (take place of) *ingia mahali pa*; (prosper) *fanikiwa*, *pata*, *faulu*, *wa na mwisho mwema*, *tokea vema*, *kunjuka*. Succeed in, *wesa*, *pata*, *jaliwa*, *faulu*.

Succeeding, a. -a *pili*, -a *baadaye*.

Success, n. (result) *mwisho*; (good fortune) *mwisho mwema*, *bahati njema*, *kufanikiwa*, *njia*, *heri*.

Successful, a. -a *kufanikiwa*, -a *heri*, &c.

Succession, n. *kuingia mahali pa*, *haki ya kushika kazi ya*; (series) *kufuatana*, *mafuatano*, *mwandamano*. A succession of events, *mambo mengi yakifuatana* [*yakiandamana*], *utaratibu wa mambo*.

Successive, a. -a *kufuatana*, -a *kandamana*, -a *baadaye*.

Successively, adv. *kwa kufuatana*, *moja kwa moja*.

Successor, n. *afuataye*, *aingiaye mahali pa mtu*, *ajaye nyuma*, *mwandami*, *badala*; (heir) *mrithi*.

Succinct, a. -a *maneno machache*.

Succinctness, n. *kutumia maneno machache*.

Succour, v. *msaada*, *shime*, *auni*.

— n. *sayidia*, *leta shime*, *pigania*, *tia nguvu*, -pa *moyo*.

Succulent, a. -enyi *maji mengi*, -a *utomvu mwingi*.

Succumb, v. *shindwa*, *jitoa*, *patwa*, -fa.

Such, a. *hivi*, -a *ginsi hii*, *sawa*, -a *namna hiyo fullani*, *kama hiyo* [*huyu*, &c.], -*lioanana*, -a *mfano mmoja*; (remarkable) -*kubwa*, -*ingi*, *ajabu*. Such a thing, *habari hiyo*.

Such and such, *fullani*. He is such an ass, *kweli ngamia huyu*.

Such a business, *jambo kama nini*.

Such as, *kama*, *methili ya*. Such that, *hatta*.

Suok, v. *fyonda*, *fyonza*; (the breast) *nyonya*; (get information from) *sua*. Suck in, Suck up, -*nywa*; (as a pump) *vuta* [*kwa bomba*].

Sucker, **Suckling**, n. *mnyonya* [*wa-*]; (of plant) *mche* [*mi-*], *kitawi* [*vi-*].

Suckle, v. *nyonyesha*.

Suction, n. *kufyonda*, &c.; *kuvuta kwa bomba*, *mvuto* (*Taz. Suck*).

Sudden, a. -a *gháfala*, -a *tháruba moja*. On a sudden, *gháfala*, *marra*.

Suddenness, n. *gháfala*, *kuwa gháfala*.

Sudorific a. [*dawa*] *ya kutoza jasho*.

Suds, n. *posu ya sabuni*.

Sue, v. *taka*, *omba*; (prosecute) *shtaki*, *dai*.

Suet, n. *shahamu ya nyama*, *mafuta*.

Suffer, v. (endure) *vumilia*, *stahimili*, *chukua*; (allow) *acha*, *kubali*, *ruhusu*; (feel pain) *umwa*, *umizwa*, *teswa*, *ona uchungu*; (be damaged) *pata hasara*, *haribika*, *hasirika*; (be affected) *patwa*, *tendewa*; (be punished) *patilizwa*, *rudiwa*, *athibishwa*. You will suffer for it, *utaona wee*, *utalipa*.

Sufferance, n. *kuachiwa*, *ruhusa*; (endurance) *uvumilivu*.

Sufferer, n. *mwenyi hasara* [*shari*, *taabu*, *huzuni*, *maumivu*, &c.], *mteswa*, *maskini*.

Suffering, n. *umivu* [*ma-*], *kuteswa*, *mateso*, *uchungu*, *taabu*.

Suffice, v. *tosha*, *kifu*, *faa*, *rithisha*, *wesa*.

Sufficiency, n. *kutosha*, *utoshelevu*, *uwezo*; (store, stock) *akiba*, *mali*; (independence) *ukinaifu*.

Sufficient, a. -a *kutosha*, &c. (*Taz. Suffice*). It is sufficient, *bassi*, *bassi tena*.

Sufficiently, adv. *kadiri ya kutosha*, *kadiri*.

Suffix, n. [(Gram.) *sehemu ya neno yenye kutiwa mwishoni*, *baada ya Root*].

Suffocate, v. *songa roho*, *songa nyonga*, *suia pumuzi*.

Suffocation, n. *kusonga* [*kusongwa*] *roho*, &c.

Suffragan, a. (bishop) *askofu mdogo*.

Suffrage, n. [*uwezo wa kuchagua mtu kuwa mkuu au kuwa katika baraza kuu ya serkali*]; (opinion, vote) *mapenzi, shauri, neno, chaguo* [*ma-*]; (witness, approval) *ushuhuda, ukubali*; (short prayer) [*sala fupi*]. Universal suffrage, [*watu wote kuwa na Suffrage*]. Household suffrage, [*wenyi nyumba kuwa na Suffrage*]. To be elected by universal suffrage, *kuchaguliwa na watu wote*.

Suffuse, v. *funika, jaza, enea katika*.

Suffusion, n. *kufunika*, &c.

Sugar, n. *sukari*; (brown, half-made) *sukari guru*.

— v. *tia sukari*.

Sugar-cane, n. *mua* [*miwa*].

Sugary, a. *-a sukari, kama sukali, -tamu*.

Suggest, v. *onya, tia moyoni, toa shauri, penyesha habari*; (give idea of) *dokeza*; (by signs) *ashiria, pungia*.

Suggestion, n. *onyo* [*ma-*], *shauri* [*ma-*], *dokezo* [*ma-*], *ishara*.

Suggestive, a. *-a kuonya, -a maana*.

Suicidal, a. *-a kujifisha, -a kujiangamiza, -a kujiletea hasara*.

Suicide, n. *kujifisha makusudi*. Commit suicide, *jifisha, jiuu, jithalimu nafsi*.

Sui generis, a. *-a peke yake, -a mti-ndo, -a namna*.

Suit, n. (of clothes) *kisua*; (in law) *madai, uda'wa, mashtaka, hukumu, maneno*; (request) *haja, maombi*; (of marriage) *kupoza, mapozo*.

— v. *faa, stahili, saki, stahiki, -wa sawa* [*-suri*], *wajibu*; (agree) *patana, lingana*. Suit oneself, *chagua -enyewe*. Suit each other, *chukuana*.

Suitability, n. *kufaa*, &c.

Suitable, a. *-a kufaa*, &c. (*Taz. Suit*, v.).

Suite, n. [*jamii ya wafuasi wa mtu*

mkuu], *wafuasi*; (series, set) *jamii, mafuatano*.

Suitor, n. *mchumba* [*wa-*], *mwenyi kupoza, mpozaji, mpozi*; (in law) *mdai* [*wa-*].

Sulk, v. *kuwa Sulky, nuna*.

Sulkiness, n. *uchungu, ukaidi, chuki*.

Sulky, a. *-enyi uchungu, -kaidi, -a kununa, -nuni*.

Sullen, a. *-enyi uchungu, -kaidi*; (gloomy, heavy) *-zito*.

Sullenness, n. *kuwa Sullen*.

Sulphate, n. (of copper) *mrututu*; (of magnesia) *chumvi ya haluli*.

Sulphur, n. *kiberiti*.

Sulphurous, a. *-a kiberiti*.

Sultan, n. *sultani, mfalme, jumbe* [*ma-*].

Sultana, n. *malkiya, mkewe sultani*.

Sultanate, Sultanship, n. *usultani, &c*.

Saltriness, n. *kuwa Sultry*.

Sultry, a. *-a hari, -a jua kali, -liokauka, -kavu*; (oppressive) *-a kusonga, -a hewa nzito*.

Sum, n. (total amount) *jumla*; (in arithm.) *hesabu*; (of money) *fetha*; (meaning) *maana*. A sum of money, *fetha*. Pay a large sum, *lipa fetha nyingi*.

— v. *hesabu*. Sum up, *jumlisha, fanya muhtasari, sema kwa vichache*.

Summarize, v. *jumlisha, sema kwa maneno machache, fanya muhtasari*.

Summary, n. *muhtasari*.

— a. *-a marra moja, -a gháfula, -a tháruba*. In a summary manner, *upeski, kwa haraka, billa kufikiri, marra moja*.

Summer, n. *wakati wa jua kali, wakati wa hari*; (in south latitudes) *kaskazi, musimi, chaka*.

Summer-house, n. [*kibanda cha anasa bustanini*].

Summersault, n. = **Somersault**.

Summit, n. *kilele* [*vi-*]; (tip) *ncha*; (highest point) *upeo, juu*. On the summit of, *juu ya*.

Summon, v. *ita*; (prosecute) *peleka*

- sheriani* [kwa kathi], dai. Summon for debt, -wiwisha.
- Summons**, n. *mwito, kwitwa hukumu*.
- Sumpter**, a. [nyama] -a kazi.
- Sumptuary**, a. -a kupunguza gharama, -a kuzuia anasa.
- Sumptuous**, a. -a anasa nyingi, -a thamani, -zuri sana.
- Sumptuousness**, n. *kuwa Sumptuous*.
- Sun**, n. *jua* [ma-], *kama jua*.
— v. *anika juani*. Sun oneself, *ota* [jiota] *jua*.
- Sunbeam**, n. *mwanga wa jua, kianga*.
- Sunburnt**, a. -*ekundu* [-kavu] *kwa jua, -liokauka*.
- Sunday**, n. *Juma a pili*, [siku ya *Bwana*].
- Sunder**, v. *tenga, pasua, kata*.
- Sundries**, n. *takataka, vitu vingi*.
- Sundry**, a. -*ngine, kathawakatha, baathi*.
- Sunfish**, n. [samaki ya mviringo].
- Sunflower**, n. [ua kubwa].
- Sung**, pf. t. ya Sing.
- Sunk**, pf. t. ya Sink, v. A sunk fence, [shimo refu lenyi ukuta upande mmoja], *handaki*.
- Sunless**, a. *pasipo jua, -a giza*.
- Sunny**, a. -a *jua, -a hari*; (joyous) -a *furaha, -kunjufu*.
- Sunrise**, n. *kucha, jua lichapo, macho ya jua, mapambazuko, jua likipanda*. From sunrise to sunset, *mchana kuchwa*. From sunset to sunrise, *usiku kucha*.
- Sunset**, n. *magharibi, jua likishuka, machweo, kuchwa*.
- Sunshine**, n. *jua, mwanga wa jua*; (after rain) *kianga*.
- Sunstroke**, n. *kupatwa na jua*.
- Sup**, v. -la *chakula cha jioni*.
- Superabundance**, n. *wingi, masazo, maziada*.
- Superabundant**, a. -*ingi mno, -a kusasa*.
- Superannuate**, v. [ondosha katika kazi kwa sababu ya kupita umri wa karuni].
- Superannuation**, n. *kuondosha, (neut.) kuondoka, &c. (Taz. Superannuate)*.
- Superb**, a. -*zuri sana, bora*.
- Supercargo**, n. *karani, msimamizi wa shehena*.
- Supercilious**, a. -*juvi, -a kitongotongo, -a kiburi, -a kutharau, -a kujivuna*. A supercilious look, *kutazama kijuvi, macho ya kiburi*.
- Superciliousness**, n. *kuwa Supercilious*.
- Supererogation**, n. [kupita kadiri watu wapaswavyo kwa haki], -a *sayidi*.
- Superficial**, a. -a *Superficies, -a kijuujuu*; (hasty, careless) -a *haraka, -a kutaghafali, -a purukushani*. Treat superficially, *purukusha*. A superficial wound, *jeraha ndogo* [ya nje, ya ngozini tu].
- Superficies**, n. *upande wa nje* [wa juu], *sura ya juu, eneo*.
- Superfine**, a. -*zuri sana*.
- Superfluity**, n. *usazo* [ma-], *masidio, baki, kisicho na kazi, wingi*.
- Superfluous**, a. -a *burre, -sio na kazi, -siotumika, -a kupita kiasi, -a sayidi*.
- Superhuman**, a. -a *kupita binadamu, -kubwa* [-ingi] *mno, -a Muungu*.
- Superincumbent**, a. -*liowekwa juu, -a juu*.
- Superintend**, v. *simamia, angalia, amuru kazi*.
- Superintendence**, n. *usimamizi, madaraka, matengenezo, maangazi*.
- Superintendent**, n. *msimamizi, mwangalizi* [wa-].
- Superior**, a. -a *juu, -ema sayidi, -kubwa, bora, -a kupita -ngine*.
- Superior to**, -*sioshindwa na, kupita, zaidi ya*.
- Superiority**, a. *kuwa Superior*.
- Superlative**, a. *bora mno*. In a superlative degree, *kupita yote*.
- Supernal**, a. -a *juu*.
- Supernatural**, a. *si -a ulimwengu, si -a ginsi ya viumbe vyote, -a ku-*

- pita asili. si kwa desturi ya vitu vyote, si kama vitu vinginevyo, si -a dunia hii, -a ajabu; (spiritual) -a rohani, -a Muungu: (miraculous) -a mwujiza. The supernatural, yasiyoonekana, yapitayo asili yetu.*
- Supernumerary**, n. [*zayidi ya hesabu iliyoamriwa*], *akiba.*
- Superpose**, v. *weka juu.*
- Superposition**, n. *kuweka [kuwekwa] juu.*
- Superscribe**, v. *andika juu, tia anwani.*
- Superscription**, n. *anwani, andiko la juu.*
- Supersede**, v. (take the place of) *ingia mahali pa, -wa badala ya; (remove) ondosha, batilisha tangua.*
- Supersensual**, a. [*-sioonekana na macho ao masikio*], *-a kupita akili, -a kiroho.*
- Superstition**, n. *imani ya uwongo, dini ya ujinga, ibada ya kishenzi [kuabudu pepo, sanamu, miungu ya uwongo, &c.]; kufanya upuzi kama uchawi, uchaji mwingi mno katika mambo ya dini [kupiga bau, kutazama ndege, kuwaa hirizi, kuangalia chuo, &c.].*
- Superstitious**, a. *-a Superstition.*
- Superstructure**, n. *ujenzi wa juu.*
- Supervene**, v. *tukia baadaye, fuata, tokea, zukia.*
- Supervis**, v. *simamia, angalia, amuria.*
- Supervision**, n. *usimamizi, maangazi, madaraka, amri.*
- Supine**, a. (on the back) *chali; (slack) -legevu, -zito, -zembe.*
- Supineness**, n. *ulegevu, &c.*
- Supper**, n. *chakula cha jioni.*
- Supperless**, a. *pasipo Supper.*
- Supplant**, v. *twaah mahali pa, ondosha, punguza [poteza] kidogo kidogo kwa siri.*
- Supple**, a. *-a kupindikapindika, -a kunyumbuka, -liopindikana, -epesi, laini; (yielding) -a tabia laini, -tii.*
- Supplement**, n. *maongezo, utimizo [ma-], nyongeza.*
- Supplementary**, a. *-a kuongeza, -a kutiniliza, -a zaiiai.*
- Suppleness**, n. *kuwa Supple.*
- Suppliant, Supplicant**, a. *-a kuomba, ombi, -ombaji.*
- Supplicate**, v. *omba, sihi, taka, lalama.*
- Supplication**, n. *maombi, haja, kuomba.*
- Supplicatory**, a. *-a kuomba.*
- Supplies**, n. *matumizi, akiba, kandi, masarufu, vyakula, riziki, nafuu, vyombo, vifaa.*
- Supply**, n. *kutoa, kuleta, kuweka; (store, quantity) wingi, akiba, jami, auni; (public) fetha ya serikali. Supply and demand, [kadiri ya kutaka na ya kupatikana itakwayo, mali na tamaa]. (Taz. Supplies.)*
- v. *toa, leta, weka, -pa, auni, ruzukisha; (on credit) kopesha. Supply the place of, -wa mahali pa, -wa badala ya.*
- Support**, n. *kuchukua, &c. (Taz. Support, v.); (prop) tegemeo, nguzo, mhimili [mi-], [kitu chenye kazi ya kuchukua, &c., mti, kibau, chakula, fetha, riziki, &c.]; (help) msaa, shime, upendeleo. Means of support, riziki, chakula, nafuu.*
- v. (bear) *chukua, tegemea, himili; (endure) vumilia; (help) sayidia, fariji, -pa moyo, pendelea, burudisha; (maintain) lisha, chukua, patia chakula; (a cause) shindania, shika; (continue) endeleza, dumisha, fuliza; (attest) shuhudia, thubutisha; (attend) fuatana na, sindikiza. Support life on, ponea, -la. How does he support himself? anaponea nini, apataje riziki?*
- Supportable**, a. *-a kuchukulika, -a kuvumilika.*
- Supporter**, n. *mtu wa kuchukua, &c., msayidia, mfuasi.*
- Supposable**, a. *-a kuwazikana, yamkini.*
- Suppose**, v. (consider) *wasa, thani, ona; (fancy, guess) tunga, baha-*

tisha, gisi; (require) *hitaji, taka*.
 Suppose that, Supposing, *ikiwa, labuda, kwamba, iwapo*. Suppose they differ, *hatta na waachane*.
Supposition, n. *wazo* [ma-], *thana*; (not fact) *hadithi, maneno, uwongo*.
Supposititious, a. -*liotiwa kwa hila, -a hila, -a uwongo, si halisi*.
Suppress, v. (overcome) *shinda, vunja, komesha*; (restrain) *funga, zuia*; (conceal) *ficha, setiri*.
Suppression, n. *kushinda, &c.*
 Suppression of urine, *kufunga mkojo*.
Suppressive, a. -*a kushinda, &c.* (*Taz. Suppress*).
Suppurate, v. *fanya usaha, tunga usaha*.
Suppuration, n. *kutunga usaha*.
Supremacy, n. *ensi kuu, mamlaka, uweso, kutawala, hukumu, nguvu*.
Supreme, a. -*kubwa sana, bora halisi, -zuri kabisa*. The Supreme Being, *Muungu Mwenyezi*.
Supremely, adv. *kupita yote, xayidi, haswa*.
Sure, a. (certain) -*a hakika, yakini*; (positive) -*a kujua sana*; (trustworthy, safe) *amini, thabiti, salama, imara*; (confident) -*enyi tumaini, pasipo shaka*. You are sure to go, *huna buddi utakwenda*. Be sure, Feel sure, (have no doubt) *yakinia, jua sana, tumaini sana*; (be beyond doubt) -*wa yakini* [hakika]. Make sure, *hakiki, hakikisha*. Yes, to be sure, *ndio, kweli, na'am, eewalla*.
Surely, adv. *hapana shaka, hakuna buddi, haikosi*; (safely) *salama, kwa hathari*.
Surety, n. *mthamini, lazimu*.
Suretyship, n. *uthamini*.
Surf, n. *mawimbi* [yakifanya pofu], *mawimbi meupe, mawimbi ya kuumka*.
Surface, n. *upande wa nje, upande wa juu, juu, sura, uso*. Surface of the earth, *uso wa arthi, sura ya inchi*.

Surfeit, n. *shibe, wingi*.
 — v. *shibisha, vimbisha, kinaisha*.
Surge, n. *mawimbi* [ya povu, ya kuumka].
 — v. *inuka, fanya mawimbi, umka*.
Surgeon, n. *mganga* [wa-].
Surgery, n. *uganga*; (room) *chumba cha kazi ya mganga*.
Surgical, a. -*a mganga*.
Surliness, n. *ukali*.
Surly, a. -*kali*.
Surmise, v. (judge) *thani, waza*; (guess, fancy) *tunga, bahatisha*.
 — n. *wazo* [ma-], *thana*.
Surmount, v. *pita juu, pita, shinda*.
 Surmounted by, -*enyi juu yake*.
Surmountable, a. -*a kupitika, -a kushindika*.
Surname, n. [jina la pili, jina la mwisho, jina la kuonyesha jamaa].
 — v. *tia Surname*.
Surpass, v. *pita, shinda, zidi*. He surpasses him in power, *amemzidi kwa nguvu, amemzidia nguvu*.
Surpassable, n. -*a kupitikana*.
Surplice, n. [nguo nyeupe ya wafanyao kazi ya dini kanisani].
Surpliced, a. -*enyi Surplice*.
Surplus, Surplusage, n. *baki, sazo, salia* [ma-].
Surprise, n. (feeling of wonder) *mshangao, kustaajabu*; (thing) *shani, kizushi, ajabu*; (bewilderment) *fathaa*; (sudden onset) *kugundua, kugunduliwa*. Take by surprise, *jia kwa hila, fumania, gundulia, zuka*. Cause surprise, *shangaza, kang'a, stusha, ajabisha, tia kishindo*.
 — v. *ajabisha, shangaza*; (bewilder) *kang'a, kang'anya, fathaisha, stusha*.
Surprising, a. -*a ajabu, &c.* (*Taz. Surprise, v.*).
Surrender, v. *toa, salimisha*, (neut.) *jitoa, shindwa*.
 — n. *kutoa, kutolewa, &c.*
Surreptitious, a. -*a hila, -a siri*.
Surround, v. (be, go round) *xunguka, -wa mzingo wa* [pande zote za, kandokando la]; (place round)

- zungushia*; (besiege) *husuru, fanyia mazingiwa*.
- Surtout**, n. [*vazi kama joho*].
- Surveillance**, n. *usimamizi, mangazi, ulinzi, kuchunguliwa*.
- Survey**, v. *tazama, kagua, chungulia, angalia*; (measure and describe exactly) [*andika sura halisi kwa kupima na kuhesabu*], *pima, kadirisha*.
- n. *kutazama, &c.*
- Surveying**, n. *kutazama, &c.* (*Taz. Survey*, v.); (map-making) [*maarifa ya kupima inchi ao bahari na kufanya ramani, kupima inchi*].
- Surveyor**, n. [*mwenyi kazi ya Surveying*].
- Survival**, n. *kuishi baada ya kufiwa, &c.*; (remainder) *baki, masalia*.
- Survive**, v. *ishi baada ya kufiwa, zidi kukaa*; (be saved) *okoka, pona katika hatari*; (remain) *baki, salia*.
- Survivor**, n. *mwenyi Survival, mwenyi kuokoka*.
- Susceptibility**, n. *wepesi wa kuona* [*kustuka, kupata, kupatwa, &c.*]; (kindness) *huruma, utu mwema*.
- Susceptible, Susceptive**, a. *mwenyi Susceptibility*.
- Suspect**, v. *shuku, tuhumu, thania viovu*; (fancy) *thani, gisi, waza*.
- Suspend**, v. (hang) *tundika, angika*; (balance) *ning'iniza*; (defer) *weka. ahirisha*; (stop work, &c. of) *zuia kazi ya, uzulu, toa, tangua*.
- Suspend a sitting**, *vunja baraza*.
- Suspend payment**, *filisika*. **Suspend judgement**, *kaa na mashaka*.
- Suspense**, n. *mashaka, kusitasita*; (pause, stop) *kukoma*.
- Suspension**, n. *kutunaika, kutungika, &c.* (*Taz. Suspend*). **Suspension bridge**, [*daraja la kitundika kwa kamba, minyororo, &c.*].
- Suspensory**, a. *-a kuchukua*.
- Suspicion**, n. *kuthania viovu, tuhumu* [*ma-*], *mashaka, shuku* [*ma-*].
- Suspicious**, a. *-enyi kuthania viovu, -enyi mashaka*; (untrustworthy) *si amini, si wazi, si -nyoju*.
- Sustain**, v. *chukua, tegemea, sayi-*
- dia*; (prove) *thubutisha*; (endure) *patwa na, vumilia*; (allow) *kubali, tia ithini*.
- Sustenance**, n. *vyakula, makuli, riziki, nafuu*.
- Sustentation**, n. *kulisha, kusayidia, kuendeleza, kuchukua, kutegemea*.
- Sutler**, n. *mchuuzi* [*kwa asikari*].
- Sutling**, n. *kazi ya Sutler*.
- Suture**, n. *kushona* [*kwa mganga*], *kiungo*.
- Suzerain**, n. *mkuu, bwana, seyidi*.
- Suzerainty**, n. [*uwezo na kazi ya Suzerain*].
- Swab**, n. [*kitani ao kitambaa wa kupangusia*].
- Swaddling-clothes**, n. [*vitambaa vya kumfungia kitoto, nguo za kitoto*].
- Swagger**, v. *tamba, jipotoa, enda kwa kujivuna*; (make a show) *piga makuu, fanya fahari, fanya jeuri, jijetea maume*.
- n. *majivuno, makuu, ufithuli, jeuri*.
- Swahili**, n. *na a.* (person) *mswahili, [wa-]*; (language) *kiswahili*.
- Swain**, n. *mtu wa shamba, mkulima*; (lover) *mchumba* [*mwanaume*].
- Swallow**, n. (bird) *barawai*.
- v. *meza, -la yote*; (put up with) *vumilia*; (recant) *jikania, jikatalia, geuza*; (take on trust) *sadiki marra moja pasipo shaka*.
- Swam**, p. t. *ya Swim*.
- Swamp**, n. *ziwa* [*la maji na matope mengi*].
- v. *jaza maji, toza majini, pindua*; (ruin) *angamiza, pindua*.
- Swampy**, a. *-enyi Swamps, kama Swamp, -a majimaji, -a matope mengi*.
- Swan**, n. [*ndege kama bata kubwa sana*].
- Sword**, n. *majani* [*mazuri madogo*].
- Swarm**, n. *kundi, kundi sima, kundi la nyuki*.
- v. *fanya kundi kama nyuki, songana, -wa -ingi, -jaa, -saa sana*.

Swarthiness, n. *weusi*.

Swarthy, a. *-eusi* [*uso, ngozi*].

Swathe, n. (of grass, &c.) *fungu, chungu*.

Sway, v. (move to and fro) *sukasuka*; (swing) *pembeza, ning'inisha*; (neut.) *ning'inia, wayawaya, tiki-sika*; (stagger) *levyalevyu, sitasita*; (influence) *geuza, vuta, ongoza, tawala, weza*.

— n. *kuning'inia, &c.*; (rule) *utawala, uwezo wa mfalme, enzi*; (power, influence) *nguvu, mvuto, mwendo wa nguvu*.

Swear, v. (p. t. **Swore**, pf. t. **Sworn**) *apa, laani, tukana*; (cause to swear) *apisha, funga kwa kiapo*. Swear at, *tukana, laani, apiza*. Swear in (soldiers, &c.), *changa kwa kiapo*. Swear by, *apa*; (trust in) *amini, jetea, tegemea*. Swear eternal friendship, *chanjiana*. Swear mutually (to each other), *apiana*. Swear solemnly (on the Book), *apa* [*piga*] *yamini* [*Koran*]. Cause to swear, *apisha, afya*.

Swearer, n. *mtukana, mnajisi wa maneno*.

Swearing, n. *kuapa, laana, matukano, maapizo*.

Sweat, n. *jasho, hari, vukuto*.

— v. *toa* [*toza, toka*] *jasho*; (of exaction) *toza* [*watu*] *faida vibaya, onea*.

Sweaty, a. *-a Sweat*, n.

Sweep, v. (p. t. *na* pf. t. **Swept**) *fagia, takasa*; (empty) *fanya -eupe* [*tupu*]; (remove) *chukua, risha, ondoa -ote, futia mbali*; (clear out) *kumba*; (move proudly) *pita kwa nguvu* [*kwa fahari*]; (survey) *pisha jicho juu ya, tazama -ote*; (of musical instrument) *pisha mkono juu ya, piga*. Sweep away, *futia mbali, ondoa -ote, pangusa, kumba*.

— n. *kufagia, mfuto, &c.*; (of arm, arms) *pigo la gháfala*; (range) *eneo, upeo, pigo*; (direction) *maelekeo*; (current) *mwendo wa nguvu, mvuto*.

Sweep up (in heaps), *zoa*. Make a clean sweep, *kumba, futia mbali*.

Sweepings, n. *takataka, matakata*.

Sweepstakes, n. *tuzo la jumla, tuzo kubwa*; (contest) *kushindania tuzo kubwa, shindano kuu*.

Sweet, a. *-tamu, -a kupendeza, laini, -zuri*; (to smell) *-a kunukia*; (water) *baridi*. Of his own sweet will, *kama apendavyo mwenyewe tu*.

Sweeten, v. *tia utamu, tia sukali, fanya tamu, kolea*.

Sweetheart, n. *mchumba* [*wa-*].

Sweetmeat, n. *maandasi matamu*.

Sweet-potato, n. *kiazi* [*vi-*].

Sweets, n. (pleasures) *utamu, furaha*; (bonbons) *maperementi, sukali, vitamu*.

Swell, v. (pf. t. **Swelled**, **Swollen**) *vimba, tuna, umka, fura*; (increase) *zidi, ongezeka*; (spread) *tanuka, enea, unka*; (be proud) *jivuna*; (be full of) *ingiwa na . . . -ingi*; (cause to swell) *vimbisha, zidisha, &c.*

— n. *kuvimba, kuzidi*; (waves) *mawimbi ya mkoba*; (fop) *mmalidadi* [*wa-*].

Swelling, n. *uvimbe, kivimbi*; (protuberance) *nundu, kitumbo*; (increase) *maongezo, maziada*.

— a. *-a kiburi, -a kuiwuna, -a kuunka*.

Swelter, v. *legea* [*shindwa, zimia*] *kwa hari*.

Swerve, v. *geuka, kwenda upande*; (incline) *inamia*.

Swift, a. *-epesi, -a mbio, -a marra moja, -a haraka, -a gháfala*; (ready, prompt) *tayari*.

Swiftly, adv. *upesi, hima, kwa haraka*.

Swiftness, n. *wepesi*.

Swill, v. (drink) *-nywa kwa pupa*; (pour on) *mwagia maji tele, suza*.

Swim, v. (p. t. **Swam**, pf. t. **Swum**) *ogolea, elea, chukuliwa na mkondo*; (move smoothly) *pita upesi*; (be dizzy) *ona kizunguzungu*; (cause to swim) *eleza, ogelesha*; (pass by swimming) *vuka kwa kuogelea*.

Swimmer, n. *mwogelea*.

Swimming, n. *kuogelea, &c.* (*Taz.*

- Swim**); (dizziness) *kizunguzungu*.
- Swimming**, a. -a *kuogelea*, -a *kuelea*; (dizzy) -a *kizunguzungu*; (tearful) -a *machози*.
- Swimmingly**, adv. *upesі, vizuri, rahisi*.
- Swindle**, v. *punja, kopa, danganya, karamkia*.
- n. *kukopa, ukopi, ujanja, uthalimu, hila*.
- Swindler**, n. *mkopi, ayari, wjanja, mthaliimu*.
- Swine**, n. *nguruwe, jamii yanguruwe*.
- Swing**, v. (p. t. na pt. t. *Swung*), (rock) *ning'inia, pembea, wayawaya*; (be hung) *tundikwa*; (move to and fro) *sukasuka, jongea huko na huko*; (move aside or round) *enda upande, enda kuzunguka*; (set swinging) *ning'iniza, pembeza, jongeza huko na huko, zungusha kwa nguvu*, (neut.) *sukasuka*.
- n. *kuning'inia, &c.*; (rope-swing) *pembea*; (sweep, rush, range, &c.) *pigo, mwendo wa nguvu, mshindo, njia, eneo*. Be in swing (in full swing), -wa *katika kutenda kazi yake, enda, sitawi*. Give full swing to, *endesha, sitawisha, sizuia*.
- Swinish**, a. *kama nguruwe, -chafu*.
- Swipe**, v. (cricket) *piga kwa nguvu*.
- Switch**, n. *ufito [fito]*; (points on railway) *panda la njia [ya gari la moshi]*.
- v. *geuza njia, geuza upande*.
- Swivel**, n. [*pete yenyi kuzunguka*].
- Swollen**, pt. t. ya *Swell*, v.
- Swoon**, n. *kuzimia roho*.
- v. *zimia roho*.
- Swoop**, n. *ruka chini [kama tai]*.
At one swoop, *tharuba moja*.
- v. *ruko [la kuja chini], ruko la ghafala*.
- Swop**, v. *badili*.
- Sword**, n. *upanga [panga]*; (curved) *kitara [vi-]*; (short, straight) *shime*. Put to the sword, *ua, chinja*.
- Sword-fish**, n. *papa upanga*.
- Swordsman**, n. [*mtu hodari kwa upanga*], *asikari wa upanga*.
- Swore, Sworn**, p. t. na pf. t. ya *Swear*.
- Swum**, pf. t. ya *Swim*.
- Swung**, p. t. na pf. t. ya *Swing*, v.
- Sybarite**, n. [*mtu wa anasa nyingi*].
- Sycamore**, n. *mkuyu [mi-]*.
- Sycophancy**, n. [*mambo ya Sycophant*].
- Sycophant**, n. *msifu mbaya, mjite-ndekeza vibaya, mstahifu mno*.
- Syllabic**, a. -a *Syllable*.
- Syllable**, n. [*harufu yenyi sauti moja, jamii ya harufu yenyi kutamkwa pamoja*].
- Syllabus**, n. *muhtasari*.
- Syllogism**, n. [*hoja halisi isiyokanikana*].
- Syllogistic**, a. -a *Syllogism*.
- Syllogize**, v. *tumia Syllogism*.
- Sylph**, n. [*kijana mwanamke mwe-mbamba mzuri*].
- Sylvan**, a. -a *mwitu*.
- Symbol**, n. *mfano, alama, dalili, ishara, methali, onyo*; (creed) *kanuni ya imani, shahaaa*.
- Symbolic, Symbolical**, a. -a *mfano, &c. (Tax. Symbol)*; (significant) -enyi *maana*.
- Symbolism**, n. *mifano, kutumia mifano*.
- Symbolize**, v. *onya kwa Symbol, fanana na, -wa kama*; (hold same creed) *patana, -wa na imani moja*.
- Symmetrical**, a. -enyi *Symmetry*.
- Symmetry**, n. *ulinganifu, uzuri, kadiri, usawa*.
- Sympathetic**, a. -a *huruma, &c.*
- Sympathize**, v. -wa *na huruma*.
- Sympathy**, n. *huruma, upole, utu mwema*.
- Symphony**, n. *ulinganifu wa sauti nyingi, uimbo*.
- Symposium**, n. *kula bia, karamu, kikao, jamii ya watu wakila pamoja*.
- Symptom**, n. *alama, ishara, dalili, onyo [ma-], kicnyo, shuku*.
- Symptomatic**, a. -a *kuonya*.
- Synagogue**, n. [*kanisa la kiyahudi*].
- Synchronism**, n. *wakati mmoja, mwaka mmoja, ulinganifu wa wakati, usawa wa miaka*.

Syncope, n. *kuzimia, kulegea, kama kufa*.

Syndicate, n. [*shirika la watu wenyi kazi moja*], *kampani*.

Synod, n. [*mkutano wa wakubwa wa kanisa*].

Synodic, Synodical, a. -a **Synod**.

Synonym, n. [*neni lenyi maana ile ile na jingine*], *maana sawa*.

Synonymous, a. -enyi maana moja, -a kuonya kitu kile kile, -a kuhuzika na.

Synopsis, n. [*habari nyingi kwa maneno machache, maneno ya kujumlisha maarifa*], *muhtasari, ukumbusho, jumla*.

Synoptic, a. -a **Synopsis**, -a **Synoptist**.

Synoptists, n. [*Mattayo, Marko, Luka, waanjilisti*].

Syntax, n. [*elimu ya kupanga maneno kwa sarufi*].

Synthesis, n. [*kutia pamoja, kufanyisa vitu vingi kuwa moja, kuinganisha, kuchanganya, kulinganisha*].

Synthetic, a. -a **Synthesis**.

Syphilis, n. *sekeneko, kijeraha cha mboni, tego*.

Syphon, n. = **Siphon**.

Syria, n. *Sham*.

Syringe, n. *bomba ndogo*.

Syrup, n. *asali, kama asali, [dawa nzito tamu ya kunywa]*.

System, n. (orderliness) *utaratibu, ukamilifu, kawaida, desturi*; (series, group) [*jamii ya vitu vyenye hali moja au kazi moja au kuwiana*], *jamii nzima*; (entire plan) *mambo yote, habari zote*; (plan, method) *shauri, madaraka, matengeneo, njia*; (body) *mwili, maungo*.

Systematic, a. -a **System**.

Systematize, v. *andika kwa System, panga, tengeneza*.

T.

Tabby, a. (of cat) [*-a madoadoa, -a milia meusi na meupe*].

Tabernacle, n. [*hema ya ibada au*

masikani ya Wayahudi, patakatifu; kisanduku kitakatifu].

Tabernacle, v. *tua, kaa*.

Table, n. *meza*; [*kitu chembamba sawa laini, mti, madini, cho chote*]; (food) *chakula*; (list, index, scheme) *muhtasari, hesabu, dafitari, jumla la habari*. Turn the tables, *badilisha hali*. At table, *chakulani*. Table-cloth, *nguo ya meza*.

Tableau, n. *taswira, sanamu, mfano*.

Table d'hôte, n. [*kula pamoja wageni katika Hotel*], *kula bia*.

Table-land, n. [*inchi sawa iliyo-inuka*].

Table-spoon, n. *mwiko mkubwa*; (as measure) *nussu wakia (l'az. Spoon)*.

Tablet, n. *kibau cha kuandikia*.

Taboo, v. *harimisha, kataza, gombeza kabisa*.

Tabour, n. *kigoma*.

Tabular, a. -a **Table**, *kama Table, wazi, -a taratibu*.

Tabulate, v. *andika wazi [taratibu], fanya muhtasari [hesabu]*.

Tacit, a. -a *kimya, -liothihirika pasipo kunena*. He gives a tacit consent, *hakatai*.

Taciturn, a. -nyamavu, -a *kimya, -a maneno machache, -stirifu*.

Taciturnity, n. *unyamavu, &c.*

Tack, v. (of ship) *bisha, kisi matanga, pindua demani [goshini]*; (in sewing) *piga bandi*.

— n. *msomari mdogo*; (of ship, tacking) *mbisho*; (course) *majira*; (change) *ugeuzi, upinduzi*.

Tackle, v. *kamata, shikilia*.

—, **Tackling**, n. *vyombo [vya jahazi, kamiba, ayari, &c.], pambo*.

Tact, n. *werevu, akili, busara*.

Tactical, a. -a **Tactics**.

Tactician, n. [*mjuzi wa Tactics, mwalimu wa mambo ya vita*].

Tactics, n. *maarifa ya vita*.

Tadpole, n. [*mdudu mdogo wa maji*].

Tag, n. [*kipande kidogo nchani*].

Tail, n. *mkia [mi-], upande wa*

mwisho [wa kinyume]. Turn tail, *kimbia*. Put tail between the legs, *fyata mkia*. Wag the tail, *sukasuka mkia*.

Tailor, n. *mshoni* [wa-].

Taint, n. (blemish) *waa* [ma-]; (disgrace) *aibu*; (smell) *uvundu*, *kioza*; (infection) *ugonjwa*, *kiambukizo*.

— v. *ambukiza*, *haribu*.

Tainted, a. *-enyi* **Taint**, n.

Take, v. (p. t. Took, pf. t. Taken) *twa*, *shika*, *kamata*; (convey) *chukua*, *peleka*; (please) *pendeza*; (choose) *chagua*; (require) *hitaji*, *taka*; (use) *tumia*; (remove) *toa*; (receive) *pokea*; (endure) *vumilia*; (understand) *fahamu*; (accept) *kubali*. Take a bite, *mega*, *ambua*. Take a walk, *tembea*, *enda tembea*. Take as spoil, *teka*. Take an oath, *apa*. Take across, *vukisha*, *vu-sha*. Take aim, *piga shebaha*, *lekeza bunduki*. Take after, *fanana na*, *iga*, *fuatisha*. Take at one's word, *sadiki*, *kubali*. Take away, *chukua*, *ondoa*, *toa*. Take breath, *pumzika*. Take by force, *nyang'anya*, *poka*. Take care, *angalia*, *tunza*, *jihathari*. Take down, *shusha*, *tweza*, *tungua*, *tundua*; (building) *bomoa*; (in writing) *andika*; (fruit, &c.) *angua*. Take effect, *tenda kazi yake*, *faa*. Take the fancy, Take the eye, *vuta*, *pendeza*, *tamanisha*, *tazamisha*. Take fire, *waka*. Take heart, *jipa moyo*, *piga moyo konde*. Take heed, *angalia*, *jihathari*. Take hold (of), *shika*, *shikilia*, *kamata*. Take in, (understand) *fahamu*; (cheat) *punja*; (include) *weka*, *-wa na . . . ndani*; (lessen) *punguza*; (water) *vuja*; (undertake) *jipatia kazi ya*; (buy regularly) *jinunulia marra kwa marra*. Take in hand, *shika*, *jitia katika*, *maliki*. Take into one's head, *azimu*, *nia*. Take in vain, *taja burra*, *tharau*. Take leave of, *aga*, *agana na*. Take medicine,

